CHUO CHA BIBLIA.

Waamuzi, Ruthu na I & II Samweli

Kitabu Cha Masomo # 3

Kitabu Cha Waamuzi

SURA YA KWANZA.

Masumbufu ya Uasi

Kitabu cha Waamuzi kinajumuisha muda wa miaka mia nne ya historia ya Wayahudi. Aya ya kutanguliza kitabu hiki cha Waamuzi inazungumzia juu ya kifo chake Yoshua na upungufu wa uongozi uliofuatia kutokana na kifo chake. Yoshua hakufanikiwa kumtayarisha kiongozi ambaye angeshika ushukani baada ya kifo chake. Na kwa ufupi, kitabu hiki cha Waamuzi kinazungumzia juu ya kuadhirika kwa taifa la Israeli kutokana na kushidwa kwa Yoshua kumtayarisha kiongozi mrithi wake kwa niaba yao. Kote kati kitabu hiki cha Waamuzi, tutatambua kwamba hawa waamuzi wote walishindwa kuwatayarisha viongozi watakaofuata baada yao na kuyaendeleza maono yao na kuhusu jinsi ambavyo watu wake Mungu walitakikana kuongozwa.

Msitari mkuu katika kitabu cha Waamuzi unatueleza kwamba hapakuwepo na mfalme katika Israel nyakati hizo za historia yao, na kwamba, *'Kila Mtu alilitenda hayo aliyoyaona kuwa ni mema machoni pake mwenyewe.'* (Waamuzi 17:5-7). Wasomi wengi wakubaliana kwamba mwandishi wa kitabu hiki alikuwa ni Nabii Samweli. Na kwa sababu hapakuwa na mfalme nyakati zile katika siku zao waamuzi, hivyo basi yawezekana kwamba mwandishi wa kitabu hiki alikiandika nyakati za himaya ya uongozi wa kifalme. Nyakati hizi za waamuzi zilikuwa siku za giza kuu katika historia yao Wayahudi kabla yao kuwa naye mfalme.

Ujumbe muhimu wa kiroho tunaopokea katika Waamuzi ni ule ambao unahusika na jambo lile linalotajwa kama 'Uasi.' Neno 'Uasi,' ni neno ambalo asili yake ni 'Kusimama kando na au mbali na.' Wakati mwingine, neno hili humaanisha, 'kuanguka' kutoka kwa imani. Katika sura ya kumalizia ya kitabu cha Yoshua, wana wa Israeli walikuwa wamejitolea na kuyaweka maangano na kwa njia ya imani kuifanya nadhiri au ahadi yao. Yoshua alisema*, 'Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia Bwana, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana.'* Wao kwa njia nyingine waliweka nadhiri mbele na katikati yake Yoshua naye Mungu, *'sisi nasi tutamtumikia Bwana, maana yeye ndiye Mungu wetu. Tumechagua kumtumikia na kumtii Mungu.'* Hii ndiyo iliyokuwa nadhiri au ahadi yao.

Wao walichagua kumtumikia Mungu, na wakaufanya ule msimamo kwa ajili yao binafsi na kwa niaba ya jamii zao. Uasi kwa msemo mwepesi ni: Unauchukua msimamo kama wana wa Israeli

walivyofanya, halafu baadaye unasimama kando na msimamo ule, au unauweka kando msimamo wako mbali na nadhiri na kujitolea kwako kwake Mungu.

Mviringo au Duara la Uasi.

Katika kitabu cha Waamuzi, tunaona mviringo au duara ya uasi ambao wana Waisraeli walipitia kwa nyakati saba na kwa muda usiozidi miaka mia nne. Kama ukiwazia juu ya uso wa saa ya ukutani inayotueleza masaa na sekunde, mviringo huu wa uasi unaanza na ule mkono wa kuonyesha saa ukionyesha saa sita. Huu ni mfano wao wana Waisraeli wakati Mungu anapoichukua nafasi ya kwanza na wao wanaambatana na matakwa yake Mungu. Saa saba ni ishara kwamba wana wa Israeli wanasimama kando mbali na kule kujitolea kwao kwake Mungu. Saa nane ni ishara kwamba upo utovu wa tabia ukifuatiwa na utovu wa kisiasa saa tisa. Saa kumi, adui muovu mno atokea. Saa kumi na mbili wana wa Isreali wanatekwa naye yule adui. Wakati mkono wa saa unazunguka kuonyesha saa kumi na mbili, wana wa Israeli ni watumwa wake yule mtekaji wao.

Mkono wa kuonyesha saa unapozidi kuelekea upande ule mwingine, saa moja upo ufufuo au mwamsho wa kiroho. Watu wamlilia Mungu naye anawarehemu. Saa mbili Mungu anamwinua kiongozi ambaye anamwita, na kumtayarisha na kumpa changa moto ili aongoze mageuzi na kumwondosha yule mtekaji mwovu. Huyu kiongozi anapewa jina 'Mwamuzi.' Saa tatu huyu mwamuzi anaanza kukusanya vyombo pamoja nao watu wakumwondoa na kumfukuza huyu mtekaji muovu. Saa nne mageuzi yanatimizwa na ushindi mkuu unashuhudiwa saa tano. Baada ya ushindi na kumfukuza yule mtekaji, wana wa Israeli wanarudi tena saa sita, wakimtumikia na kumpenda Mungu kwa mara nyingine tena.

Kwa vipindi tofauti vya wakati, yote yaonekana kuwa swali-hadi wakati ule ambao unaposoma haya maneno: *'Kisha wana wa Israeli walifanya yaliyo maovu mbele za macho ya Bwana.'* Na hapo ndipo tunapotambua kwa mara nyingine kwamba mviringo au duara lile la uasi linaanza kuzunguka tena– na tena– na tena. Wana Waisraeli walikuwa na amani kwa wakati baada ya nyakati za kunusurika kwa miaka themanini kwa wakati moja, lakini hata hivyo, mara mara kwa mara, uasi ulitokea na mzunguko ule ukashuhudiwa kwa vipindi vingine saba.

Kuna mambo mawili ambayo tunajifunza na kupokea katika kitabu hiki cha Waamuzi. Kwanza, kuna mambo ambayo tunastahili kutimiza ambayo ni ya kibinafsi. Je! Kuna uwezekano sisi kusimama kando na au mbali pamoja na kuanguka kutokana na yale tunayoamini wenyewe? Je!

Inawezekana kuasi? Kitabu cha Waamuzi kinatuonyesha kwamba jambo hili lina uwezekano wa kutokea.

Tunaonywa katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati na pia kutoka kwa mtume Paulo hivi, *'Yeye ajidhaniaye amesimama (kuendelea) ajihadhari asije akaanguka.'* Uhakika kwamba tayari tumeingia katika Nchi Ya Ahadi huko Kanaani na kuitwaa hakumaanishi kwamba hatuwezi kusimama kando mbali na, au kuanguka mbali kutokana na yale ambayo tunaamini. Kitabu cha Waamuzi kinatuonyesha kwa mara nyingine kwamba wana Waisreali walianguka mbali kwa kuasi wao. Na vile vile kama wao, sisi sote tunazo nyakati ambazo huziweka ahadi na nadhiri kuu kwake Mungu, na hata hivyo bado huwa tunasimama au kuanguka mbali katika maagano yetu naye Mungu. Na wakati ambapo tunafanya hivyo, ni lazima tuilipie gharama kuu ya kuasi kinyume na Mungu.

Funzo lingine kwetu ambayo tunahitajika kulitimiza kutoka kitabu hiki cha Waamuzi ni lile ambalo tunaweza kulitaja kama 'uasi wa kitaifa.' Jinsi ambayo wana wa Waisraeli walipitia hiyo duara mara nyingi katika kitabu cha Waamuzi, kuna uwezekano kwa mataifa mengine kupitia duara hiyo kwa siku hizi za leo pia.

Kulikuwepo wakati Nchi Takatifu ilikuwa ndiyo 'Makao Makuu yake Mungu,' na Yerusalemu ulikuwa ndio mji mkuu wa kiroho wa ulimwengu. Lakini, viongozi wa kiroho walimpatia Mungu kisogo na kumkataa Yesu Kristo na wito wake wa Kimasihi. Wakati Yesu alipoingia Yerusalemu Jumapili ya kwanza ya mitende, alisema haya maneno kwao viongozi wa kidini, *'Kama hamtayazaa matunda ya ufalme wake Mungu, Mungu atauchukua ufalme kutoka kwenu na kuwapa watu ambao watayazaa matunda hayo.'* Kwa maneno mengine, Mungu ataamisha Makao Yake Makuu. Kama ile nchi haizai matunda ya ufalme wake Mungu, Yesu alisema kwamba, *'kujitolea kwake Mungu ni kama kuliangukia jiwe. Naye aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika-vunjika'; naye ye yote ambaye litamwangukia, litamsasa tikitiki.'* (Mathayo 21:42-44).

Wakati Yesu alipouchukua ufalme kutoka kwao viongozi wa kidini wa Israeli, aliupatia kanisa Lake. Hii nikumaanisha mafunzo haya kutoka kitabu hiki cha Waamuzi kuhusu somo hili la duara hii ya uasi linaelekezwa kwa Kanisa Lake. Na kwa sababu iko tafsiri moja peke yake bali njia tofauti za matimizo ya maandiko, maonyo haya kuhusu uasi yanaweza kutumika kwa huduma zote kama jinsi ambavyo yaweza kutumika kwa taasisi za Biblia, pamoja na vyuo ambavyo misingi yake ilikuwa ni kulifundisha neno lake Mungu.

Ni lazima tuyatilie maanani maonyo yale ambayo yanahusu uasi katika kitabu hiki cha Waamuzi, kwetu binafsi, na kwa mashirika yale tunayohusika nayo, pamoja na mataifa yetu. Ujumbe wa kitabu hiki ni kwamba kila mara tushike ushukani 'Saa Sita,' katika upendo, kuabudu na kumtumikia Mungu.

SURA YA PILI

Mambo Yasiyo ya Kawaida Kuwapitia Watu wa Kawaida

Ya ziada katika onyo zilizo katika kitabu hiki cha Waamuzi, ni kwamba kuna mafunzo mengi ya kiroho ambayo yanatokana na maisha ya hawa Waamuzi. Hawa waamuzi ni miongoni mwa mifano bora ya kitabia tuwezayo kujifunza katika maandiko.

Othnieli ndiye aliyekuwa mwamuzi wa kwanza. Kulingana na maandiko, hati ya kumthibitisha huyu Othnieli na ya kipekee ni kwamba yeye alikuwa binamu yake Yoshua. Na hati ya kitambulisho ambayo mwamuzi wa pili, Ehudi alikuwa nayo ni kwamba yeye aliutumia mkono wa kushoto kwa ustadi mkuu. Tunazidi kuelezwa kwamba sifa za mwamuzi mwingine, Debora, zilikuwa kwamba yeye alikuwa mama tu huko Israeli. Naye alikuwa na wakati mgumu akimtafuta shujaa wa vita, Baraka ili aupokee ujasiri na kuandamana naye vitani. Gideoni alipoitwa, yeye alisema, *'Ee, Mungu, nitawaokoa Israeli kwa jinsi gani? Tazama, jamaa zangu ndio walio maskini sana katika Manase, na mimi ndimi niliye mdogo katika nyumba ya baba yangu*.' (Waamuzi 6:15). Hili ni wazo kuu ambalo laonekana kote kwao hawa waamuzi, kwamba wao ni watu walio wakawaida tu.

Je! Wewe wajidhania kuwa mtu wa kawaida na asiye na lo lote la muhimu? Na Je! Wewe waamini kwamba Mungu hawezi, au hataweza kukutumia wewe kwa kuwa hauna kipawa au uwezo wa kutimiza yaliyo makuu kwake Mungu? Kitabu hiki cha waamuzi kitakuonyesha kwamba Mungu hupendezwa na kuyafanya mambo yasiyo ya kawaida kupitia watu wa kawaida kama mimi na wewe.

Othnieli alikuwa ni mwana wake Kenazi, ndugu mdogo wa Kalebu. Biblia inasema haya kumhusu yeye: *'Roho ya Bwana ikamjilia juu yake, naye akawa mwamuzi wa Israeli; akatoka kwenenda vitani, naye Bwana akamtia huyo Kushan-rishathaimu, mfalme wa Mesopotamia, mkononi mwake; na mkono wake ukamshida Kushan-rishathaimu.'* (Waamuzi 3:10).

Mungu hupenda sana kuwatumia watu wa kawaida na kutenda mambo yasiyo ya kawaida kuwapitia wao kwa kuwa Roho Wake anawaongoza. Hili ndilo jambo ambalo linatajwa katika Agano Jipya kama kujazwa naye Roho Mtakatifu.

Jambo hili tunaliona pia kwake mwamuzi aliyeitwa Ehudi ambaye hati ya kitambulisho chake ilikuwa tu kwamba yeye ni mtu aliyeutumia mkono wa kushoto. Israeli ilikuwa chini ya utumwa wao Wamoabu. Mfalme aliyeitwa Egloni alikuwa amewateka. Wakati taifa linapoliteka taifa lingine nyakati zile, liliwaweka wao wale waliotekwa chini ya kongwa au mzigo mzito wa kulipia ushuru. Ehudi alikiongoza kikundi ambacho kilisafiri hadi mji mkuu wa Moabu ili kulipa ushuru kwa niaba ya Israeli yote. Ehudi aliingia katika jumba lake mfalme na kulipa ushuru wao. Lakini kabla ya kuaza hiyo safari ya kuelekea huko kwa mfalme, Ehudi alijifanyia upanga uliokuwa na makali kuwili, urefu wake ulipata dhiraa moja; akaufunga huo upanga ndani ya nguo yake katika paja lake lamkono wa kuume.

Huku akisimama mbele yake mfalme Egloni, aliyekuwa amewanda sana. Naye hap[o alipokuwa amekwisha kuisongea hiyo tunu, *'Mimi nina ujumbe utokao kwa Mungu kwako wewe.'* Tunazidi kusoma kwamba, na kwa mkono wake uliokuwa wenye nguvu nyingi na wa kushoto, aliuvuta huo upanga kuutoa hapo katika paja lake la kuume, akamtia tumboni mwake; hicho kipini nacho kikaingia ndani pamoja na huo upanga wenyewe. Ehudi alianza mageuzi nao Wamoabu wakabanduliwa kutoka kwa uongozi wao wakimabavu. Jambo ambalo tunaelezwa kumhusu huyu Ehudi ni kwamba yeye alikuwa ni mtu mwenye kushoto. Na inawezekana kwamba kitu kile ambacho Ehudi angeweza kumpatia Mungu na cha kipekee ni huu mkono wake wa kushoto. Naye Mungu aliutumia huo mkono kwa njia kuu. Je! Wewe umevitoa vipawa vyako vidogo na vikuu kwake Mungu? Ikiwa utavitoa vipawa vyako vionekanavyo kuwa vidogo kwake Mungu, Yeye atavitumia jinsi alivyotumia mkono wa kushoto wake Ehudi.

Hadithi moja ya kuvutia kati ya hawa wakombozi ni yake Debora, mama moja huko Israeli. Huyu Debora alikuwa na kipawa au karama maksusi ya kiroho. Yeye alikuwa nabii. Aliketi chini ya mtende wa Debora, katika nchi ya vilima vilima ya Efraimu; wana wa Israeli wakakwea kwake, awaamue.

Siku moja akamzungumzia mtu moja aliyeitwa Baraka*, 'Je! Mungu wa Israeli, hakutoa amri, akisema, Enenda, ukawavute kwako, huko katika mlima wa Tabori, watu elfu kumi wa wana wa Naftali, na wana wa Zabuloni? Nami nitakuvutia Sisera, amiri wa jeshi lake Yabini, hata mto mwa*

Kishoni, pamoja na magari yake, na wingi wa watu wake; nami nitamtia mkononi mwako?' (Waamuzi 4:5-7).

Baraka akamwambia, *'Kama utakwenda pamoja nami ndipo nitakwenda; bali kama huendi pamoja nami, mimi siendi.'* (Waamuzi 4:7-8). Baraka alifahamu kwamba kama kwa hakika Mungu alikuwa akinena naye kumpitia huyu Debora, basi Mungu angalifanya yeye kuwa mshindi. Ili kumjaribu huyu Debora, na kuona kana kwamba yeye mwenyewe aliamini kwamba huu ulikuwa ni ujumbe wake Mungu, kwa hivyo, ndipo akamwambia, *'Wewe andamana nami. Safiri nami.'* Debora akakubali, lakini akamwonya kwamba, *'hakika safari utakayoiendea haitakupatia heshima wewe;maana Bwana atamwuza Sisera katika mkono wa mwanamke'* (Waamuzi 4:9-10) Wakati ambapo Baraka aliwatangazia wana wa Israeli kujitokeza ili kwenda vitani, watu wapatao elfu kumi walijitokeza. Na hili ndilo lile ambalo huyu Debora alimweleza kwamba lingelitukia.

Hii vita ilipiganiwa juu ya mlima Tabori. Mungu akamfadhaisha Sisera na magari yake yote, na magari yake yote, na jeshi lake lote, kwa makali ya upanga, mbele ya Baraka; basi Sisera akashuka katika gari lake, akakimbia kwa miguu. Mwanamke mmoja jina lake Yaeli akajitolea ili kumficha Sisera katika hema lake. Sisera akashikwa nao usingizi mzito kwa haraka na uchovu mwingi mno na huku akiwa amelala fo fo fo, huyu Yaeli akatwaa kigingi cha hema, akashika nyundo mkononi mwake, akamwendea polepole, akamtia kile kigingi katika kipaji chake, nacho kikapenya, hata kuingia mchangani.

Kumbuka, ujumbe mkuu katika kitabu cha Waamuzi ni kuhusu uasi pamoja na matokeo yake. Hata hivyo, pia tunajifunza kutoka maisha yao hawa waamuzi kwamba Mungu huwatumia watu duni. Yeye hupendezwa na kuwachukua watu wa kawaida kama mimi na wewe na kutenda mambo yasiyo ya kawaida kuwapitia. Mungu hufanya mambo ya ajabu kupitia watu wa kawaida na ambao wanaongozwa naye Roho Mtakatifu.

SURA YA TATU.

Kila Mtu Kwenye Doria lake

Gideoni ndiye mwenye kuvutia zaidi miongoni mwa waamuzi wote. Tutamtazama kwa karibu mno kwa kuwa maisha yake yana mengi ya kutufundisha sisi sote. Kwa mfano, kama wewe haujidhamini vyema, hebu yatilie maanani yale ambayo huyu Gideoni anayoyasema mwenyewe:

'Jamaa zangu ndio walio maskini sana katika Manase, na mimi ndimi niliye mdogo katika nyumba ya baba yangu.' Yeye aliishi nyakati za watu wakatili mno–Wamidiani waliokuwa wamewateka Waisraeli nyakati zile. Wengi wa wana wa Israeli waliangamia katika vita vyao na Wamidiani na mazao ya mimea yao yalifanyiwa uharibifu mkuu, hivi kwamba hawakuwa na cho chote cha kula.

Baada ya miaka saba ya umasikini na ukatili, watu wa Israeli walimlilia Bwana Mungu awape msaada. Mungu naye akamwita mtu ambaye angefanyika mkombozi wao. Mtu huyo alikuwa ndiye Gideoni.

Tunasoma kwamba malaika wake Bwana Mungu alishuka na kuketi chini ya mti wa mwaloni uliokuwa huko Ofra, na ni mali yake Yoashi. Mwanawe Gideoni alikuwa akipepeta ngano yake ndani ya shinikizo ya mvinyo kwa kuwa alikuwa akiificha ile ngano machoni pa Wamidiani. Malaika wake Bwana akamtokea na kusema, *'Bwana yu pamoja nawe, Ee shujaa*.' Majibu yake Gideoni kwa hayo maneno yalikuwa ni haya, *'Ee Bwana wangu, ikiwa Bwana yu pamoja nasi, mbona mambo haya yote yametupata? Yako wapi matendo yake ya ajabu, waliotuhadithia baba zetu..?*' (Waamuzi 6:12-13).

Miaka mingi ilikuwa imepita tangu wakati ule walipovuka bahari ile ya Shamu naye Gideoni alitaka kufahamu ikiwa Mungu angali akiwapa watu wake miujiza jinsi alivyofanya nyakati zake Musa. Malaika wake Mungu alimwelezea Gideoni kuwa ikiwa angaliuona mwuijiza ambao Mungu angaliutumia ili kuwakomboa wana wa Israeli kutoka kwa Wamidiani, ilimbidi yeye ajitazame kwenye kiio. Tunaona mkazo wa funzo kuu kwa mara nyingine. Mungu kwa mara nyingine atapendezwa kumchukua yeye aliye duni na mwenye kutoka kabila lililo hafifu na maskini na kumtumia ili kuyatimiza mambo makuu na yasiyo ya kawaida na ya kimwuijiza aliyopanga kwa ukombozi huu.

Ni jambo la muhimu wakati Mungu anapokuita wewe kumtendea kazi, kuiendea kazi yake ukifahamu kwamba ndiye aliyekutuma na yupo pamoja nawe. Na ni lazima ujifunze siri fulani zake Mungu ambazo hawa waamuzi na wakombozi wengine kama Musa walijifunza. Siri hizo za kiroho ni hizi: Haijalishi wewe ni nani au una cheo gani; bali kwamba ni yale ambayo Mungu anaweza kutenda. Haijalishi yale ambayo wewe unataka kutenda; bali ni yale Mungu anataka kutenda ambayo ni muhimu. Na wakati mwuijiza utakapotendeka, wewe utatazama hapo nyuma baadaye na kusema, *'Siyo yale mimi niliyotenda; bali ni yale ambayo Mungu alitenda kwa kuwa alikuwa amenituma Mimi, na kwamba Mungu alikuwa pamoja nami.'*

Mungu hawatafuti watakatifu wasio wa kawaida. Yeye kwa kawaida anawatafuta wale walio duni miongoni mwao wadhaifu, kwa kuwa hawa ndio rahisi kwao kujifunza hizo siri za kiroho ambazo Musa na viongozi wengine wake Mungu walijifunza. Je! Watu wanaweza kujifunza siri hizi kama wao ni watakatifu wasio wa kawaida? Kwa hakika wao watajitengemea kwanza kabla ya kumtengemea Mungu. Lakini ikiwa wao ni duni miongoni mwa waliodhaifu, ni hakika kwamba Mungu anaweza kuwafanya kumtumainia yeye. Mtu wa aina hii ndiye Mungu alimwinua mara nyingine na nyingine katika kitabu hiki chao Waamuzi.

Mungu alipomwita huyu Gideoni kuwapindua hawa Wamidiani, kulikuwepo na maelfu yao Wamidiani. Wao walikuwa kama baa la nzige kwa jinsi walivyokuwa wengi. Ilimbidi Mungu aithibitishe imani yake Gideoni. Mungu hutaka kumpa mtu vitu viwili wakati anapoijenga na kuithibitisha karama ya imani yake. Jambo la kwanza Mungu hutaka kuthibitisha imani yake yule mtu kupitia majaribu. Mungu pia hutaka kujithibitisha kwake mtu yule. Hebu tazama jinsi ambavyo Mungu ataithibitisha imani yao watu wakati ambapo anajaribu kuwaita wao kutenda jambo fulani ambalo linahitaji imani kuu. Zaburi 37:23 inasema hivi *'Hatua zake mtu zaimarishwa na Bwana.'*

Wengi wetu tunafahamu vyema hadithi kuhusu ngozi ya kondoo yake Gideoni. Mungu alimwita Gideoni afanyike mkombozi wa Israeli kutoka kwa Wamidiani. Gideoni alihitaji uhakikisho kwamba Mungu alikuwa akimwita yeye na kwa sababu hiyo, akamwuliza Mungu amthibitishie. Usiku ule akaichukua ngozi akaiweka katika kiwanja cha kupuria; na kama ikiwapo umande juu ya ngozi tu, na nchi yote ikiwa kavu, basi hapo ndipo atakapojua ya kuwa utawaokoa Israeli kwa mkono wake kama alivyosema. Gideoni alipoamkia asubuhi yake, alipata hivyo, maana alikamua ile ngozi, akautoa ule umande katika ile ngozi, bakuli nzima ya maji. Hata hivyo, akawa angali hajaridhika, usiku uliofuatia akamwuliza Bwana sasa ngozi iwe kavu na umande juu ya nchi, yote. Asubuhi iliyofuatia nchi ile ilikuwa na umande juu yake na ngozi ilikuwa kavu.

Na kwa sababu Mungu alikuwa akimwita huyu Gideoni kuitenda kazi kuu mno, yeye alitenda jinsi ambavyo alivyomtaka kutenda. Lakini tunahitajika kuwa waangalifu wakati ambapo tunapomtaka Mungu ajidhihirishe kwetu sisi. Kuna msitari mwembamba sana kati ya kumwekea Mungu ngozi jinsi Gideoni alivyofanya na kumweka Mungu katika majaribu. Wakati Yesu alipojaribiwa huko jangwani, yeye alipewa changa moto ajitupe chini kutoka sehemu ya juu zaidi ya Hekalu. Na kama malaika wangalimwokoa, kila mtu angalifahamu kwamba yeye ni mwana wa Mungu. Lakini Yesu akasema,

'Imeandikwa, usimjaribu Mungu wako.' Sisi humwendea Mungu kwa njia ya imani. Kuna wakati ambapo Mungu atatujaribu sisi. Hata hivyo, sisi hatuna haki ya kumjaribu Mungu.

Unapoanza safari yako ya kiroho, ni kana kwamba unajiunga na 'Chuo Kikuu cha Imani.' Wewe hauna haki ye yote kumjaribu Mungu. Lakini Mungu ana haki ya kukujaribu wewe. Yeye aweza kukupa wewe mtihani wa 'ghafula tu' na mitihani migumu kwa majira tofauti, lakini wewe hauna haki ye yote ya kumjaribu Mungu. Mungu afahamu kwamba upo wakati ambapo wewe utakuwa umejawa nayo imani na bado wahitaji uthibitisho wa aina fulani. Hii sio sawa na kumweka Mungu katika majaribu kwa kuwa wewe hauna imani kwake yeye.

Mungu pia aliithibitisha imani yake Gideoni kwa njia nyingine. Kabla yao kuwavamia Wamidiani, ambao walikuwa wamepiga kambi kwenye wingu kuu la giza huko bonde la Yezreeli, Mungu alimwambia Gideoni kuingia kwa siri huko katika kambini yao Wamidiani. Yeye alisimama kando ya hema yao Wamidiani askari jeshi wawili na kusikiliza jinsi mmoja wao alivyokuwa akisema kuhusu ndoto yake. Alikuwa ameamka kutoka kwa ndoto yake. Aliyasema haya, *'Tazama, niliota ndoto. Na tazama, mkate wa shayiri ulianguka katika kambi ya Wamidiani, ukafika hata hema moja, ukaipiga hata ikaanguka, nao ukaipindua, hata ikalala chini*. Je maana yake yanaweza kuwa ni yapi?' *Askari mwenzake akamjibu hivi, 'Habari hii haikosi kuwa upanga wa Gideoni, mwana wa Yoashi, mtu wa Israeli. Mungu amewatia Wamidiani na jeshi lote katika mkono wake.'* (Waamuzi 7:12-14).

Gideoni aliposikia hayo aliinama chini na kumsujudu Mungu. Baadaye aliwaendea watu wake na kusema, 'Inukeni, kwa maana Bwana amelitia jeshi la Midiani mikononi mwenu.' Je! Mungu anakutayarisha kwa kazi ya imani? Je! Inawezekana kwamba sasa Mungu ataka kuitenda kazi kuu kukupitia wewe na haujamkaribia jinsi inavyotakikana ili kufahamu hivyo?

Kabla yake Mungu kumtumia Gideoni kuwapindua hawa Wamidiani, tunaona Mungu akijidhihirisha kwake huyu Gideoni kwa njia nyingi sana na za ajabu. Tunaona Mungu akidhiirisha imani yake Gideoni. Changa moto kuu ya imani yake Gideoni ni wakati Mungu alimwuliza kutoa sadaka ya fahali mkubwa wa baba yake. Babake Gideoni alikuwa ameasi na kurudi nyuma. Yeye alikuwa ameyajenga madhabahu kwa ajili ya miungu wa Baali. Mungu alimwambia Gideoni amchukue fahali huyu wa baba yake aliyekuwa bora zaidi (Katika siku ya leo tunaweza kusema kwamba kuchukua tinga-tinga lake la dola sabini na nane elfu – karibu milioni saba), aifungilie katika

madhabahu na kuiharibu. Halafu Mungu akamwambia huyu Gideoni achukue Ashera aliyotaka na kulifanya kuwa kuni ambazo zingalitumiwa katika kuiteketeza dhabihu yao kwake Mungu.

Hiyo ilikuwa ni changa moto iliyo kuu sana. Wakati mwingi katika vitabu vya Injili, Yesu angalisema hivi, 'kama wewe haupo tayari kunifanya mimi kuichukua nafasi ya kwanza, kabla ya baba yako, wewe haunihistahili mimi.' Yesu atupa sisi changa moto hii kwamba tumweke yeye katika nafasi ya kwanza kabla ya baba na mama. Haya ndiyo Mungu aliyokuwa akimwamuru huyu Gideoni kuvunja sanamu ya babake kwa njia hiyo.

Gideoni alimtii Mungu kwa ukamilifu wote. Asubuhi iliyofuatia, watu mjini walipoyaona yale yaliyotendeka kwa madhabahu ya Baali na ile Ashera iliyokuwa karibu imekatwa, waliuliza, *'Ni nani aliyeyatenda jambo hili?*' Majibu yakawajia hivi, *'Gedioni, mwana wa Yoashi, ndiye aliyetenda jambo hili.'* Na wao walitaka kumuua Gideoni kwa kuwa yeye aliikosea miungu yao ya Baali. Kwa kuwa baba yake Gideoni alimpenda mwanawe sana, aliwaambia wale watu wa mji ule, *'Je! Mtamtetea Baali? Au mtamwokoa ninyi? Yeye atakayemtetea na auawe hivi asubuhi; kama yeye ni Mungu, na ajitetee nafsi yake, kwa sababu mtu mmoja ameibomoa madhabahu yake.'* Na siku ile Gideoni akapewa jina na kuwa Yerub- Baali, maana yake, 'Mwacheni Baali ajitetee mwenyewe.'

Mungu alijithibitisha kwake Gideoni mara nyingine alipomwambia yeye alipunguze jeshi lake. Gideoni alikuwa akiongoza jeshi la askari thelathini na mbili elfu ili kuwavamia Wamidiani. Huku wakiwa njiani mwao, Mungu akasema, '*Gideoni, sasa watu hawa ni wengi mno.'* Mungu hakumtaka Gideoni kufikiria kwamba ushindi wake ulitokana na umati wa jeshi lake kubwa. Hivyo basi Mungu akamwamuru Gideoni kuwaruhusu wenye woga na ye yote yule mwenye hofu kurudi makwao nyumbani.

Unaweza kukumbak kuwa katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati, Musa aliandika sheria ambayo ilikumbana na changa moto hii wakati jeshi la Israeli lilipokuwa likielekea vitani? Askari wote wenye hofu au woga, ye yote aliyekuwa ameposana, au yule aliyekuwa amepanda hivi karibuni na hawakuwa amekula yale matunda yake. (Kumbukumbu la Torati 20:1-8) Wakati Gideoni alipowapa changa moto hii wale waliokuwa waoga na wenye hofu, yamkini watu takribani elfu ishirini na mbili walirudi makwao.

Yeye alisonga mbele nao askari elfu kumi naye Mungu akasema, ‘Gideoni, unao watu wengi mno.’ Yeye alifahamu kwamba bado huyu Gideoni angedhania kwamba ni umati mkubwa wa jeshi uliompatia ushindi wake. Mungu akamwambia Gideoni kuwaruhusu jeshi lake kushuka chini kwenye mto ili kunywa maji naye apate kuwajaribu na kuwatenga kando wale ambao wangeramba maji kwa ulimi wao, kama vile arambavyo mbwa, kadhalika kila mtu apigaye magoti kunywa. Hesabu ya wale waliokuwa wakiramba-rama wakipeleka mkoni kinywani, ilikuwa watu mia tatu. Bali wale wengine walipiga magoti kunywa maji, naye Mungu bila kusita akasema, *‘Waambie hawa waende zao; na kila mtu mahali pake*! Na kwao wale mia tatu walioramba-ramba wakipeleka mkono kinywani, nitawaokoa, nami nitawatia Wamidiani katika mikono yako.’ (Waamuzi 7:5-7).

Hawa walikuwa ni chini ya asilimia moja yao wale walioandamana naye Gideoni hapo mwanzoni. Mungu hawahitaji maelfu yao wanaomini ambao hawajajitolea. Yeye hajawahi kutenda hivyo. Mungu anahitaji kundi ndogo la watumishi waliojitolea kabisa.

Mungu alijidhihirisha kwake Gideoni kwa mara nyingine kupitia matayarisho ya vita ambapo aliwashinda Wamidiani. Ushindi wake Gideoni ulihitaji imani kuu, ujasiri mwingi na mipangilio bora. Hawa Wamidiani walikuwa wamepiga kambi kwenye bonde lenye uvuli wa giza kuu. Mungu alimwambia Gideoni awachukue watu mia tatu waliokuwa pamoja naye, na kuwagawanya katika vikundi vitatu vya watu mia moja katika kila kikundi, na kuwatenga katika sehemu tatu: Kaskazini, mashariki na magharibi kuwazunguka majeshi ya Wamidiani. Gideoni alikuwa na mwongozo uliokuwa mwafaka na sahihi, na ambao aliwapatia askari wa jeshi lake.

Haya ni mafunzo makuu kuhusu uongozi wakati Gideoni anaposema, *‘Nitazameni, mkafanye kama nifanyavyo mimi, angalieni, nitakapofika mwisho wa kambi, itakuwa, nifanyavyo mimi nanyi fanyeni kadhalika.’ (*Waamuzi 7:17). Huu ndio uongozi halisi. Hawa watu wote walijitolea kikamilifu kwake Gideoni na kwake Mungu. Katika mikono yao ya kushoto, walikuwa na mitungi ambalo lilikuwa limeifunika mienge ya moto na katika mikono ya kulia kulikuwemo na tarumbeta au baragumu. Gideoni alipowaonyesha ishara, wao walizivunja zile mitungi zilizokuwa zimefunika ile mienge ya moto na kuonyesha mienge ile mia moja. Na wao wakazipiga zile tarumbeta zao. Kisha wakapaza sauti zao wakisema, ‘*Upanga wa Bwana na wa Gideoni!’* Haya yalitendeka kutoka katika pande na sehemu tatu tofauti.

Kama wewe ungelikuwa Mmidiani, katika usingizi mzito gizani, ungefikiria kitu gani, wakati utakaposikia kuvunjika kwa mitungi mia moja, halafu uione mienge ya moto na kusikia sauti kuu za baragumu au tarumbeta na watu mia moja wakipaza sauti zao kutoka pande za kaskazini mwa kambi yenu? Halafu jambo hilo, hilo litukie tena kutoka upande ule wa mashariki na magharibi mwa kambi yenu? Kwa hakika ungefikiri kwamba jeshi kubwa lake Gideoni lilikuwa limekuzingira kila mahali.

Hawa Wamidiani walifikiria kwamba wao wamezingiriwa kote. Wao waliingiwa na hofu kuu na kwa hamaki kuu walianza kuuana wao kwa wao. Jeshi lake Gideoni liliwafukuza wao kama kundi kubwa la mifugo. Halafu wale watu waliokuwa wamerudi makwao nyumbani kutoka jeshi lake Gideoni wakajiunga na jeshi hilo la watu mia tatu na kuwaangamiza kabisa Wamidiani.

Msitari ambao unaeleza kuhusu ushindi wao unasema hivi kuhusu hawa askari mia tatu: *'Wakasimama kila mtu mahali pake kuizunguka kambi pande zote; jeshi lote (la Wamidiani) wakakimbia; nao wakapiga kelele, wakawakimbiza.'* (Waamuzi 7:21). Na kama sehemu ndogo yao hawa watu mia tatu haingefungua mienge yao, au kuzipiga tarumbeta zao na kuzipaza sauti zao kama walioshauriwa, ule mpangilio wote haungefaulu na wao wangepata maafa makubwa kutoka kwao Wamidiani.

Hii ni picha nzuri sana ya Kanisa lake Yesu Kristo siku ya leo. Kristo aliyefufuka yeye hawahitaji maelfu ya watu ambao hawajajitolea kabisa miongoni mwao wafuasi wake. Yeye anawahitaji watu wachache wenye kujitolea mhanga na wanafunzi ambao wanaweza kusimama kila moja wao katika sehemu au mahala pake. Na kama Mungu angeweza kutufanya kila moja wetu kusimama mahali au katika sehemu yake na kuvitumia vipawa au karama zetu alizotupa, po pote pale ambapo hivyo vipawa vimetufanya kuwepo pale, na kwa kujitolea asilimia mia moja (100%) kwake Yesu Kristo, hakika tungejidhiirisha kwa majeshi yote ya kuzimu.

Kumbuka kwamba msitari mkuu ambao unatufungulia kweli katika historia ya vitabu vilivyomo katika Agano la Kale unapatikana katika Agano Jipya. Mtume Paulo anatueleza tunaposoma historia ya Waebrania tutazame mifano na maonyo yaliyo ndani mwake (1 Wakorintho 10:11). Katika kitabu cha Waamuzi maonyo mengi yanakusanyika kwenye uasi mkuu wa wana wa Israeli.

Mifano inaweza kupatikana katika maisha ya Waamuzi. Wapo wengine kama Samsoni ambao ni mfano na maonyo pia. Tazama yote katika maisha yake. Mifano yote yao hawa waamuzi ni dhihirisho la kweli kuu yake Mungu kwamba yeye hupendezwa na kuwatumia watu wa kawaida ili kutenda mambo yasiyo ya kawaida na kwa Utukufu wake mwenyewe. unapoufahamu ukweli huu inatubidi kutambua kwamba uwezo wetu mkuu ni katika kujitolea kwetu kwake Mungu na kwa yale yote anayotutakia sisi kuyatenda.

Kitabu Cha Ruthu

SURA YA NNE.

Mapenzi Yaliyomo Katika Ukombozi

Huku tukiendelea katika vitabu vya historia vilivyomo katika Agano la Kale, na baada ya kuchuguza vitabu vya Yoshua na Waamuzi, sasa tunageukia kitabu cha Ruthu. Kitabu hiki cha Ruthu ni hadithi ya kuvutia mno ya mambo ambayo yalitokea 'Nyakati ambapo Waamuzi walikuwa viongozi huko Israeli.'

Hadithi hii ni kivuli kuhusu wokovu pamoja na uhusiano wetu naye Bwana Yesu Kristo. Maandiko katika Agano la Kale na Jipya yanatueleza kwamba sisi tumeposwa kwake Yesu au sisi tu 'Bibi Harusi' Wake. Kitabu hiki cha Ruthu kinawsilisha uhusiano huu wa 'Mapenzi Yaliyomo Katika Ukombozi.' Bibilia inatupasha kwa ufasaha hadithi hii:

'Ikawa zamani, za waamuzi walipoamua Israeli, kulikuwa na njaa katika nchi. Akaondoka mtu mmoja wa Bethlehemu ya Yuda, akaenda kukaa katika nchi ya Moabu, yeye na mkewe na wanawe wawili. Na jina mtu huyo aliitwa Elimeleki, na jina la mkewe Naomi, na majina ya wanawe wawili Maloni na Kilioni, Waefrathi wa Bethlehemu ya Yuda. Wakafika nchi ya Moabu, wakakaa huko. Akafa Elimeleki, mumewe Naomi; na yule mwanamke akasalia na wanawe wawili. Nao wakaoa wake katika wanawake wa Moabu; na jina la mmoja aliitwa Orpa, na jina la wa pili Ruthu. Wakakaa huko yapata miaka kumi. Wakafa na Maloni na Kilioni wote wawili; na huyo mwanamke akawa amefiwa na wanawe wawili, na mumewe pia.' (Ruthu 1:1-5).

Elimeleki, Naomi pamoja nao wanawe wawili walisafiri kwenda katika nchi ya mbali na kukumbana na mikasa mingi. Nchi ya Moabu ni ya umuhimu kwa Wayahudi kwani itakumbukwa kwamba ni uko mwana mpotevu alikotorokea. Hadithi hii kwa hakika inaenda sambamba na ile hadithi ya mwana mpotevu. Huku jamii hii potevu ikiwa katika nchi hii ya Moabu, wana wao wawili walifariki dunia. Elimeleki pia alifariki katika nchi ile. Naomi ndiye aliyebakia katika jamii ile ambayo ilikuwa imesafiri kwenda Moabu ili kuikimbia njaa iliyokuwa huko Bethlehemu ya Yuda.

Tukizidi kutilia mkazo juu ya Naomi, tunaona ramani yenye usawa na ile iliyokuwepo katika hadithi yake mwana mpotevu. Naomi akiwa katika nchi ya ugeni huko Moabu, mambo yaliandelea kuwa magumu sana. Kabla ya wana wake wawili kufariki dunia, wao walioa wanawake kutoka nchi hiyo ya Moabu; jambo ambalo lilikuwa kinyume na matakwa ya Mungu. Alisafiri huko Moabu akiwa naye mumewe pamoja nao wana wawili. Sasa yeye hana mume, hana watoto ila tu binti wakweze wawili.

Hadithi hii inaendelea hivi, *'Ndipo alipoondoka, yeye na wakweze, ili kurudi kutoka nchi ya Moabu; maana huko katika nchi ya Moabu amesikia ya kwamba Bwana amewajilia watu wake na kuwapa chakula. Basi akatoka pale alipokuwapo, na wakweze wawili pamoja naye; wakashika njia ili kurudu mpaka nchi ya Yuda.'* (Ruthu 1:7). Jinsi ilivyo, ni kama hali hii huwakuba wapotevu wote. Nyakati zote wangalipo katika nchi ya mbali ulimwenguni humu, wao husikia jinsi mambo mema na mazuri yalivyo huko nyumbani mwa mababu zao.

'Basi akatoka pale alipokuwapo, na wakweze wawili pamoja naye; wakashika njia ili kurudi mpaka nchi ya Yuda.' (Ruthu 1:7). Huku kulikuwa ni kurudi kwake binti mpotevu. Lakini kabla ya kurudi, '*Naomi akawageukia binti wakweze na kuwaambia 'Nendeni sasa mkarejee kila mmoja nyumbani kwa mamaye; Bwana na awatendee mema ninyi, kama ninyi mlivyowatendea mema hao waliofariki na mimi pia. Bwana awajalie kuona raha kila mmoja nyumbani kwa mumewe. Kisha akawabusu; nao wakapaza sauti zao wakalia.'*

Hadithi inaendelea kusema: *'Wakamwambia, La sivyo; lakini tutarudi pamoja nawe kwa watu wako. Naye Naomi akasema, Enyi wanangu, mrejee; kwani kufuatana na mimi? Je, mimi ninao watoto wa kiume tena tumboni mwangu, hata wawe waume zenu? Enyi wanangu, mrejee; nendeni zenu; kwa kuwa mimi ni mzee siwezi kupata mume tena. Kama ningesema, Natumaini; kama ningepata mume hata usiku huu, na kuzaa watoto wa kiume; je! Mngesubiri hata watakapokuwa watu*

wazima…? (Ruthu 1:11-13). Tunaona hapo mbeleni kwamba Orpa alimbusu mkwewe Naomi miguu na kurudi makwao. Lakini Ruthu akabaki naye Naomi.

Naye Naomi akamwambia huyu Ruthu, '*Tazama, shemeji yako amerejea kwa watu wake, umfuate shemeji yako.'* Mahali hapa ndipo Ruthu anaushika ushukani katika kitabu hiki ambacho kimepewa jina lake na papa hapa ndipo tunakutana na ujumbe mkuu katika hadithi hii ya mapenzi na yenye kuvutia zaidi. Ruthu akasema: *'Usinisihi nikuache, Nirejee nisifuatane nawe; Maana wewe uendako nitakwenda, Na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako waatakuwa watu wangu, Na Mungu wako atakuwa Mungu wangu; Pale utakapokufa nitakufa nami, Na papo nitazikwa; Bwana anitende vivyo na kuzidi, Ila kufa tu kutatutenga wewe nami.' (*Ruthu 1:16-17).

Ruthu alitupatia mfano bora zaidi kuhusu kujitolea na utiifu mkuu aliposema haya maneno kwake Naomi. Hizi aya mbili zinadhihirisha utiifu na mfano bora wa jinsi ya kufanya maangano bora kuhusu ndoa kati yake mume na mke. Wakati unapomwoa mtu fulani, unajitolea kumfuata po pote pale aendapo na kuishi po pote pale atakapoishi. Labda unafikiri kwamba wewe hautaungana kwa karibu na watu wa jamaa ya mke wako, lakini baada ya miaka michache, utatambua kwamba ni bora zaidi kama utaweka nadhiri na kusema, *'watu wako watakuwa watu wangu'* au sivyo utakuwa na uhusiano wenye udhaifu mwingi naye mwenzi wako.

Sehemu kuu katika kujitolea kwako ni kusema, '*Mungu wako atakuwa Mungu wangu.'* Ikiwa mna mwabudu Mungu tofauti tofauti, hamtakuwa na misingi sawa kwa dhamira zenu za kimaisha. Hii ndiyo sababu moja kuu ya kuvunjika kwa ndoa nyingi. Sababu moja ya kuwa bila dhamira sawa katika maisha ya ndoa, ni kuwa na mvutano katika ndoa. Wakati wawili wanapoipanga miradi kuhusu jinsi ya maisha yao pamoja na kutumia wakati wao, fedha na uwezo wao, ni rahisi sana kutokumbalina katika hali hiyo. Msingi ambao unaweza kuwafanya jamaa yenye kuoana kuwa na mtazamo mmoja ni katika kukiri kwao kwamba, 'Mungu wako atakuwa Mungu wangu pia.' Dhamira ya maisha yenu inatokana na uhusiano kati yako na Mungu, na kwa hivyo mtaweza kuwa na dhamira moja ya kimaisha.

Sehemu wa mwisho katika sura ya kwanza inasema hivi, *'Basi Naomi akarudi; pamoja na Ruthu Mmoabi, mkwewe; ambao walirudi kutoka nchi ya Moabu; nao wakafika Bethlehemu mwanzo wa mavuno ya shayiri.'* Sababu hii ya kuwasili huku katika majira ya mavuno ya shayiri ni muhimu mno. Hawa wanawake wawili walipokuwa wakiwasili huko Bethlehemu, Naomi alikuwa ni mfano

wake mwana wa Mungu aliyekuwa akirudi nyumbani kwa baba yake. Neema yake Mungu ilikuwa ikingoja kumpokea yeye, jinsi ile ile baba alivyotoka kwa nyumba na kumkaribisha, kumhakikishia, kumkubatia na kumkubali yule mwana mpotevu. (Luka 15:20).

Katika hadithi hii, Ruthu anawakilisha watu ambao sio wa jamii ya Mungu. Ruthu hakuwa Mwebrania. Yeye alikuwa raia mgeni. Je, Mungu anayo neema ye yote kwake mtu ambaye si mshirika katika jamii yake? Kwa hakika yeye ana neema hiyo. Neema ya wokovu, iliyotujia sisi tulipokuwa wenye dhambi, ni njia ile ile ambayo sote ilitufanya kuwa watu wa jamii yake Mungu. Na kama tutakavyo tazama, neema yake Mungu kwake Naomi na Ruthu itapatikana katika Sheria Yake.

Sheria ya kwanza yake Mungu ambayo ilimpatia neema Ruthu na Naomi inapatikana katika Walawi 19:9-10. Sheria hii, inayotajwa kama Sheria ya kukusaya au kubugabuga mavuno, ambayo inawaambia wavunaji wasiyakusanye masazo ya mavuno yaliyoanguka-anguka chini, kwa ajili ya maskini na wageni. Ruthu aliamua kwamba katika siku yake ya kwanza huko Bethlehemu angalikwenda kukusanya masazo ya mavuno huko shambani. Tunasoma haya*: 'Naomi alikuwa na ndugu ya mumewe, mtu mkuu mwenye mali, wa jamaa yake Elimeleki, na jina lake aliitwa Boazi. Naye Ruthu Mmoabi akamwambia Naomi, 'Sasa niende kondeni, niokote masazo ya masuke nyuma yake yule yuel ambaye nitaona kibali machoni pake.' Akamwambia Haya, mwanangu, nenda. Basi akaenda, akaja akaokota masazo kondeni nyuma ya wavunaji; na bahati yake ikamtukia kwamba akaifikia sehemu ya shamba iliyokuwa mali yake huyo Boazi, ambaye alikuwa wa jamaa yake Elimeleki.'* (Ruthu 2:1-3).

Kuna sheria nyingine yake Musa ni yenye msingi muhimu ambayo hutusaidia kuelewa sababu gani hii hadithi kuhusu mapenzi iko katika Biblia. Hii ni sheria ambayo imo katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati sura ya 25, ambayo inaitwa 'Sheria ya Mkombozi wa Jamii.' Sheria hii inasema kwamba, ikiwa ndugu yake mtu amefariki bila kumzalia mwana mjane wake, inambidi yule mjane asiolewe na mtu kutoka kwa jamii nyingine ile tu, kutoka kwa jamaa mmoja wa mumewe. Hii ni kwa sababu ya kuliendeleza jina lake katika Israeli. Kwa hivyo, ndugu yake mumewe ni sharti kumwoa awe mkewe. Na kama ndugu yake mumewe aliyefariki atakataa, ni lazima ampeleke kwa wakuu wa mji. (Hii ilikuwa ni sawa na kwenda mahakamani.) Na kama akiendelea kukataa mbele yao wakuu au wazee wa mji, ndipo mke wa nduguye amkaribie mbele ya hao wazee, amvue kiatu chake mguuni mwake, na kumtemea mate ya uso; kisha atajibu yule mwanamke, aseme, Mume akataaye kumjengea nduguye nyumba yake na afanywe hivi. Na jina lake katika Israeli liitwe,

Nyumba ya mvuliwa kiatu. Hii ilikuwa aibu kuu kwake yeye ambaye aliipokea sifa hii katika mila na desturi yao wana wa Israeli.

Na kwa sababu Ruthu alikuwa ameolewa na mtu Mwebrania, na kwa hali ya ndoa, yeye alifanyika kuwa sehemu ya jamii yake Mungu, taifa la Kiebrania. Na kwa wakati ambapo mumewe alipoanga dunia, na yeye hakufanikiwa kuwa nao watoto; ilifanyika kwamba huyu Ruthu ameacha kuwa mshirika katika jamii yake Mungu. Sheria ilisema kwamba anaweza kumwendea mtu wa jamaa yake mumewe aliyefariki, na kumsihi yeye kufanyika mumewe. Na kama akikataa, jambo hili lingelifikishwa katika mahakama. Na kama angalizidi kumkataa, wazee au viongozi wa mji wangalienda mbele na kuifanya sherehe inayoelezwa katika Sheria ya Mkombozi wa Kijamii.

Mtu yule ambaye alikubali kumuoa mwanamke wa aina ile ilimbidi kumfanyia mambo mawili. Jambo la kwanza, Ilimbidi KUMNUNUA yeye kwa kulipa madeni aliyokua nayo. Jambo la pili ambalo huyu Mkombozi angalitenda ni kumchukua na kumfanya mkewe. Hii ni katika kutekeleza hali ya uhusiano wa ndoa na KUMRUDISHA katika jamaa yake Mungu. Hili ndilo lililokuwa tumaini lake Ruthu alipokuwa akirudi huko Bethelehemu ya Yuda. Na ni kwa sababu hii katika sura ya pili inaanza na habari ya kusisimua kuhusu jamaa yake mumewe aliyefariki mmoja wao alikuwa ni mtu shujaa na mwenye mali nyingi, ambaye jina lake lilikuwa Boazi.

Huku hadithi hii ya mapenzi ikiendelea, tutaona picha ya neema yake Mungu kwake mwana mpotevu aliyerudi nyumbani, na neema yake Mungu kwake ambaye alimjia Mungu kwa ukombozi wake.

SURA YA TANO.

Mapenzi Mara ya Kwanza Kuonana.

Hadithi hii yake Ruthu ilitokea siku ambazo waamuzi walikuwa wakiongoza, na siku za giza kuu ya kiroho katika historia yao Wayahudi. Hadithi hii ya mapenzi ambayo inaelezwa katika kitabu hiki cha Ruthu ni picha bora kuhusu wokovu na ukombozi wetu. Ruthu, Mmoabu na binti mkwewe Naomi, ni picha ya kuvutia ya mtu ambaye si sehemu ya jamii yake Mungu. Tunamuona Mungu akidhihirisha upendo na neema yake kwake Ruthu katika ukombozi ambao unaelezwa katika sheria yake Mungu.

Ruthu alikwenda kukusanya masazo katika konde lililokuwa lake Boazi. Wakati Boazi alipowasili kuwaamkia wavunaji siku ile alimwona Ruthu na jinsi ilivyo, alivutiwa alivutiwa na urembo wake wakati huo. Naye akamwuliza mtumishi aliyewasimamia wavunaji, 'Na huyu je! Ni msichana ni wa nani?' Ni dhahiri kabisa kwamba alivutiwa na kumpenda huyu Ruthu. Maana ya jina hili Ruthu ni – 'Urembo' au 'Chipuko la Waridi.' Mtumishi wake alimjibu akamwambia jinsi ambavyo Ruthu alivyo msichana Moabi aliyerudi pamoja na Naomi kutoka nchi ya Moabu; na jinsi alivyoifanya nadhiri ya uaminifu kwa mama mkwe wake. Alimfahamisha jinsi Ruthu alivyofanyika kuwa muumini baada ya kuolewa na mumewe aliyekuwa Myahudi.

Boazi alimwambia Ruthu kubaki katika konde lake ili aweze kumpa ulinzi. Yeye alidhihirisha kwamba alimjali sana huyu Ruthu. Katika aya ya kumi, tunasoma, *'Ndipo aliposujudia, akainama mpaka nchi, akamwambia, Jinsi gani nimepata kibali machoni pako, hata ukanifahamu, mimi niliye mgeni?'* (Ruthu 2:9-11). Neno 'neema' linamaanisha 'kibali na baraka yake Mungu ambayo sisi hatuistahili.' Boazi akamwambia Ruthu kwamba alifahamu kifo cha mumewe pamoja nayo nadhiri yake kwa mama mkwe wake. Aliendelea kumwambia kwamba yeye alifahamu jinsi alivyofikia kuwa na imani kwake Mungu wa Israeli.

Naye Ruthu akasema, *'Bwana wangu, na nipate kibali machoni pako'* (Ruthu 2:12-14) Wakati wa kula chakula, Boazi alimsihi kuungana nao katika maakuli yao ya mchana. Ruthu alikula chakula kile hata akashibam hata akasaza naye Boazi akahakikisha kwamba amerudi nyumbani mwao akiwa nalo posho kubwa kutoka kwa makusanyo yake ya shayiri ya siku ile huko kondeni. Naye Boazi aliwaagiza vijana wake kutoa kidogo katika matita na kuacha aokote, bila kumkataza. Boazi kwa hakika alikuwa amepigwa mshale moyoni kwa mapenzi aliokuwa nayo kwake Ruthu.

Mapenzi Yakiwa Kinyume

Ruthu sura ya pili inamalizikia kwa kutueleza sisi kwamba Ruthu alifanya kazi kondeni mwake Boazi kwa misimu miwili ya mavuno. Hii inamaanisha yeye Ruthu alirudia matukio ya sura ya kwanza kwa miezi sita. Sura ya tatu inaanza hivi. *'Kisha Naomi akamwambia mkwewe, Je! Mwanangu, si vizuri nikutafutie raha, ili upate mema?'* Kwa maneno mengine, Naomi alisema, 'Je, nikutafutie wewe mume?' Labda Naomi alikuwa amemweleza kuhusu sheria ya kukusanya masazo na ukombozi. Hivyo basi, tunaweza kufikiria kwamba Ruthu alifahamu kuhusu sheria ya mkombozi wa jamii na kwamba Boazi alikuwa ni mtu wa jamaa yao. Boazi pamoja nao watumishi wake walikuwa wakivuna usiku ule na wao walikuwa wakilala karibu na mavuno yao wakati wote baada ya kuvuna. Naomi akamwambia Ruthu*, 'Basi wewe oga, ujipake mafuta ujivike mavazi yako, kisha uende kwenye uga; walakini usijionyeshe kwake mtu yule, ila atakapokwisha kula na kunywa. Nayo itakuwa wakati atakapolala, utapaangalia mahali alalapo, nawe uingie, uifunue miguu yake ujilaze hapo.'* Naomi alikuwa akimwambia Ruthu kumposa Boazi kwa kumsihi yeye afanyike kuwa mkombozi wa kijamii.

Na pia kulikuwa nayo sherehe ya kupepeta shayiri pale ugani. Naye Naomi alimwambia huyu Ruthu atazame ni wapi ambapo huyu Boazi angeliweka jamvi lake kwa usiku ule. 'Usiku wa manane.' Naomi akasema, *'Nenda na kujitambulisha kwake pamoja na kumposa yeye kwa kumueleza kwamba wewe wamtaka yeye kufanyika kuwa mkombozi wako wa kijamii.'* Haya hayakuwa tu mapenzi ya ukombozi ila kwamba yalikuwa ni mapenzi ya mageuzi au kinyume. Katika desturi zao huyu Boazi siye ambaye angelimposa huyu Ruthu. Ilikuwa kwamba Ruthu ndiye aliyehitajika kumposa huyu Boazi. Ni kweli kwamba walikuwepo watu wengi wa jamaa yake mumewe aliyefariki dunia. Na kuambatana nayo sheria, Ruthu alihitajika kumwendea mmoja wao na kumposa awe mkombozi wa kijamii. Yale tu Boazi alihitajika kutenda ni kumwonyesha kwamba yeye angelipenda kufanyika mkombozi wake wa kijamii.

Yale aliyoyatenda katika sura ile ya tatu yalikuwa ni ya halali kabisa. Hii ilikuwa ni nia ya kumposa huyu Boazi ili apate kuchukuwa kama mkewe. Hivyo basi, tunasoma kwamba katika usiku wa manane, huyu Ruthu alikwenda na kulala miguuni pa Boazi. Huyu Boazi naye alishtuka na kuingiwa na hofu nyingi wakati alipopata mwanamke miguuni pake. Akamwuliza yeye, *'Ama! Wewe u nani?'* Naye Ruthu akajibu, *'Ni mimi Ruthu, mjakazi wako; uitande nguo yako juu ya mjakazi wako; kwa kuwa ndiwe wa jamaa aliye karibu.'* (Ruthu 3:8-10). Boazi akajibu, *'Mwanangu ubarikiwe na Bwana; umezidi kuonyesha fadhili zako mwisho kuliko mwanzo, kwa vile usivyowafuata vijana, kama*

ni maskini kama matajiri. Basi, mwanangu, usiogope; mimi nitakufanyia yote uyanenayo; kwa maana mji wote pia wa watu wangu wanakujua ya kwamba u mwanamke mwema.' (Ruthu 3:10-11). Boazi anampa Ruthu nafaka nyinigi kulingana na awezo wake wa kubeba huku akimwambia aelekea nyumbani kwake mama mkwe.

Ukombozi Katika Mapenzi

Tumewaona hawa wapenzi wawili wakipatana, na kupendana hadi kuposana kuifikia ndoa. Na kwa sababu ya Sheria ya Kiebrania iliyomo katika Agano La Kale, tumemwona mwanamke akimposa mwanamume. Na anapotenda jambo hilo, mpenzi wake ni lazima akumbane na hali zote za kisheria. Mwanzo wa sura ya nne ya kitabu hiki, tunamwona Boazi akishughulikia mambo yote ya kisheria na wakuu au wazee wa mji ili kusifanya ndoa ile ikubalike machoni pa sheria.

Asubuhi na mapema siku iliyofuatia baada yake Ruthu kumposa, Boazi akakutana naye mtu wa jamaa yake Ruthu kumliko yeye na kumweleza kuhusu mali yake Elimeleki ambayo ilihitajika kukombolewa. Naye yule mtu akakubali kuikomboa ile mali. Lakini Boazi alipomwambia yale yanayohitajika kabla yake kuikomboa ile mali na kwamba pia ahitajika kumwoza Ruthu yule mwanamke Mmoabu, yeye alikataa kwa kuwa yeye hakutaka urithi wake kutiwa (najisi) au kuweka mawaa katika kizazi chake. Hivyo basi, Boazi akawafahamisha wakuu waliokuwepo pale kwamba yeye ataikomboa mali yote yake Elimeleki na pia alikuwa akiikomboa kwa ndoa, kwa kumwoa Ruthu yule mwanamke Mmoabu aliyekuwa mkwewe Elimeleki.

Kukomboa humaanisha 'Kununua tena' na pia 'Kurudisha.' Boazi alimkomboa huyu Ruthu kwa njia mbili. Kwanza kabisa, yeye alimrudisha kwa kuzilipa deni zake zote. Na hapo baadaye akaujenga uhusiano naye ambao ulimrudisha yeye Ruthu kwa nyumba yake Mungu.

Katika sura ya tano katika kitabu cha Ufunuo, kuna picha nyingine ya kuvutia sana kuhusu ukombozi. Huko mbinguni kuna kilio kwa kuwa hakuna mkombozi (wa kijamii) ambaye aweza kuivunja ile mihuri katika vitabu vile hata kumkomboa mwanadamu. Halafu baadaye wale waliomo huko mbinguni wenye kulia waambiwa kwamba wasilie zaidi kwa kuwa yupo mkombozi anayestahili na mwenye upendo mkuu wa kuwakomboa wao. Mkombozi huyo ni Yesu Kristo.

Je, tumaini letu ni lipi wakati tunapotambua kwamba sisi tunahitajika kuupokea ukombozi? Tumaini letu kuu la wokovu misingi yake ni imani yetu katika kifo na ufufuo wake Yesu Kristo. Kifo

chake Kristo ndicho gharama iliyotakikana kulipwa ili kununua sisi tena katika jamii yake Mungu. Nacho kifo chake Yesu Kristo kinamaanisha kwamba yawezekana kwetu sisi kuwa na uhusiano naye aliyefufuka, na ambaye anaishi, yaani Yesu Kristo na hii inafananishwa na uhusiano wa ndoa katika Agano la Kale na Jipya. Uhusiano huu huturudisha sisi katika ushirika pamoja naye Mungu, na kudhibitisha msimamo wetu kama wana wake Mungu. Pia, huturudisha sisi katika jamii yake Mungu.

Hapo mwanzoni, Mungu pamoja na mwanadamu walikuwa katika uhusiano mkamilifu ambao ungalifananishwa kwa kukumbatiana kwa mikono pamoja. Kitabu cha Mwanzo kinatueleza kwamba Mungu alimfanya mwanadamu kiumbe mwenye uchanguzi naye mwanadamu akachagua kumpa Mungu kisogo; hali inayoeleweka vyema kwa kuachana au kutengana kukumbatiana kwa mikono. Habari njema ni kwamba Mungu alimnunua mwanadamu kupitia kifo cha Yesu Kristo juu ya msalaba, na mfano bora ni kwa kukumbatiana kwa mikono. Petro anaandika kwamba, sivyo vitu duniani, kama fedha na dhahabu, ila ni damu yenye dhamana kuu yake Yesu Kristo ndiyo ambayo ilitukumboa sisi (1 Petro 1;18-19).

Lakini hii ni sehemu nusu tu katika mwuijiza wa ukombozi. Ndoa kati yake Boazi na Ruthu inadhihirishia pande nyingine kuhusu mwuijiza huu wa wokovu. Yesu Kristo alifufuliwa kutoka kwa wafu na sasa anaugonga mlango wa mioyo yetu. Mfano mmoja wenye kuvutia sana katika Biblia, ni Picha yake aliyefufuka anayeishi na kugonga mlango wa mioyo yetu. Yeye hutuambia kwamba anataka sisi tumfungulie mlango wa mioyo yetu na kumkaribisha ili aingie ndani na kuwa nao ushirika wa karibu pamoja nasi. Yesu Kristo ndiye Bwana harusi nasi tu 'Bibi Harusi wake' katika ushirika huu. (Mathayo 25:1-13; Yohana 3:29; Ufunuo 21:2; 22:17).

Kitabu cha Ruthu ni mfano wenye utajiri mkuu na ambao unadhihirisha kweli hii. Kweli hii ndiyo tunayoitaja kama kuwa 'Mapenzi yaliyo Kinyume.' Katika mila au desturi nyingi, mwanamume ndiye mwenye kumchagua na kumposa mwanamke. Sheria hizi za ukombozi zinatumika katika hadithi hii yenye kuvutia mno ambayo inamaanisha kwamba yampasa Ruthu kumposa huyu Boazi. Nalo jambo hili pia ni la kweli kwetu sisi katika ukombozi wetu. Jambo lile tu ambalo huyu Boazi alipaswa kutenda ni kudhihirisha kwamba yeye alimpenda huyu Ruthu na angalipenda kumwoa pia. Lakini ilimbidi Ruthu kusema, 'Nataka wewe Boazi. Nakutaka wewe uwe mkombozi wangu wa kijamii! Na kwa njia hiyo hiyo wewe nami twahitajika kumkaribisha Kristo aliyefufuka, anaposimama mlangoni mwa mioyo yetu, kwa uvumilivu mwingi akiugonga, na kumwambia kwamba, 'Nakutaka wewe uwe mkombozi wangu wa kijamii! Nakutaka uninunue mimi kwako mwenyewe kupitia kifo chako juu ya

msalaba, na pia ningependa unirudishe mimi katika jamii yake Mungu na kunithibitisha katika uhusiano wa karibu pamoja nami.'

Tunapokisoma kitabu cha Ruthu kuna neno lingine lenye kuvutia mno la kibiblia ambalo tunahitajika kulitilia mkazo. Neno hili ni 'Neema.' Baada ya miaka michache katika ndoa yao Boazi na Ruthu, Mungu aliwajalia kuwa na mtoto wa kiume jina lake aliitwa Obedi. Huyu Obedi ndiye babu yake mfalme Daudi, na ambaye anamfanya Ruthu kuwa katika kizazi chake Masihi kulingana na sura ya kwanza katika kitabu cha Mathayo.

Hebu fikiria kwamba huyu Ruthu yupo mahali sokoni pamoja naye mwanawe na anawaona baadhi ya wafanya kazi ambao alikutana nao katika konde lake Boazi. Na je, kama wakimwambia yeye hivi, 'Kwa hakika wewe ulifahamu jinsi ya kumpata Boazi, kwa kujifanya mgumu na asiyepatikana kwa urahisi!' Je wafikiri huyu Ruthu angelijibu vipi kwa jambo hilo? Natumaini kuwa unaweza kumwona akikataa kwa dhati kwamba cho chote kile alichokuwa nacho kilitokana na pendo lake Boazi peke yake? Na ikiwa unamwamini wa dhati, unaweza kufikiria maelezo yake kwamba vyote vilikuwa ni sababu ya upendo wake Mungu. Hii ni pamoja na neema yake kwa mgeni kama yeye, na jambo ambalo lilifafanuliwa zaidi katika sheria ya kukusanya mavuno na ya ukombozi.

Pia unaweza vile huyu Ruthu anavyowakilisha jinsi tunavyohitajika kuwafanya wanafunzi. Ni Naomi ambaye alishiriki naye Ruthu kuhusu sheria hizi za kukusanya mavuno pamoja na Ukombozi. Naomi ndiye aliyempa ujasiri huyu Ruthu ili kuzungumza naye Boazi.

Je, wewe umekombolewa? Je, umenunuliwa kwa damu yake Kristo na kurudishwa kwake Mungu? Je, umemrudia Mungu kwa kuwa na uhusiano naye Yesu Kristo? Na je, umemkaribisha Yesu Kristo kuwa mkombozi wako wa kijamii?

Yesu anataka kuwa mkombozi wetu wa kijamii. Yeye alifanyika kuwa mwanadamu. Yesu Kristo amesimama mlangoni mwa moyo wako wakati huu. Naye anataka kuwa mkombozi wako. Ni lazima uzungumze naye ana kwa ana na kumwomba kuwa mkombozi wako. Huu ndio ujumbe ulio katika somo kuu la hadithi hii ya mapenzi na ya kuvutia ya ukombozi.

SURA YA SABA.

Ufalme Wake Mungu

Katika kitabu kinachotangulia, tulichambua sura tatu za kwanza katika vitabu vya historia vilivyomo katika Agano la Kale (Yoshua, Waamuzi, Na Ruthu), ambavyo vinavyojulikana kama 'Vitabu vya Historia yenye Mafumbo' kwa sababu ya mifano na onyo zinazotolewa ndani yake. Tunapofikia kitabu cha Samueli wa Kwanza, tunaianza sehemu ya vitabu vya historia vinavyofahamika kama 'Maandiko Ya Ufalme Vitabu Vya Historia.' Sehemu hii inahusu Samueli wa Kwanza na wa Pili, Wafalme wa Kwanza na Wa Pili, pamoja na Mambo ya Nyakati wa Kwanza na wa Pili. Vitabu hivi vyote ni 'Maandiko ya Ufalme' kwa kuwa yanaeleza kuhusu Ufalme wake Mungu. Kwa hakika, tafsiri nyingine za Biblia zinataja vitabu hivi kama Samweli wa Kwanza na wa Pili na vitabu vya Wafalme kama Samweli wa Tatu na wa Nne. Vitabu vya Mambo ya Nyakati vinarudia nyakati sawa za kihistoria, huku vikitilia mkazo jinsi ambavyo Mungu alivyoutazama wakati ule wa historia ya Waebrania.

Dhana hii ya ufalme wake Mungu ni kina kikuu katika vitabu hivi – na hivi vitabu hutusaidia kuelewa dhana hii muhimu wakati tunaposoma Agano Jipya, na hasa mno mafunzo yake Yesu Kristo. Hivyo basi, hebu tuchukue wakati na kutazama maana ya Ufalme wa Mungu katika Agano la Kale siku zile na umuhimu wake ulivyokuwa katika mafunzo yake Kristo.

Ufalme Wake Mungu Katika Agano la Kale

Chini yake Musa, wana wa Israeli walikuwa na uongozi kulingana na mapenzi yake Mungu. Bwana aliwataka wao kuishi chini ya uongozi wake Mungu. Kile kilichohitajika katika mfumo huu wa uongozi ni kuwa naye Nabii-Kuhani kama Musa (na baadaye, Samueli). Wakati Musa alipowafanyia maombezi kwake Mungu, yeye alikuwa ni kuhani (Tazama, hii mifano, Hesabu 11:1-2; 21:7). Wakati Musa aliposhuka chini kutoka mlima Sinai na ujumbe kutoka kwake Mungu kwa hao watu, yeye alikuwa ni nabii (Tazama Kutoka 20-24). Kwa wakati wote kama Mungu angelikuwa na mtu kama Musa, yeye angewatawala watu kupitia kiongozi yule. Huyu Nabii-Kuhani angalikuwa chombo cha kuyafanya mapenzi yake Mungu, naye Mungu angaliwaongoza watu wake. Huu ndio uliokuwa mpango wake Mungu kwa serikali ya watu aliowachagua.

Katika kitabu cha Samweli wa kwanza, Samweli alikuwa Nabii – Kuhani. Lakini Samweli alipozidi kwa umri nao wana wa Israeli wakawaona wana wake kuwa watu waliokosa nidhamu na stahi ya baba yao, walimwaambia Samweli kwamba wao walitaka kuwa na mfalme kama mataifa mengine (1 Samweli 8:1-5). Samweli akiwa amekatishwa tamaa alimwomba Mungu. Naye Mungu akamwaambia asidhani kwamba wao walikuwa wamemkataa. Kwa hakika watu walikuwa

wakimkataa Mungu na wala sio Samweli, huku wakimpa mfalme wa kibinadamu wadhfa wa mbele badala yake Mungu kuwa mfalme wao. Na hivyo basi, Mungu alimweleza Samweli hivi, *'Kama wao wamtaka mfalme, Samweli atawapatia wao mfalme wao!* (6-22).

Hili latuleta kwenye dhana hii kuhusu Ufalme wake Mungu. Ufalme ambao hawa watu walitaka ulikuwa, wa kitaifa, na wa kilimwengu na uliokuwa mahali dhahiri palipotambulikana na watu fulani walio dhahiri. Na kwa mfumo huu kufanya kazi, Mungu alimhitaji mfalme ambaye angalimtii. Yeye aliwahitaji makuhani ambao wangalienda mbele ya uso wake kwa niaba ya watu. Na pia aliwahitaji manabii ambao wangalizungumza kwa niaba yake Mungu kwa watu pamoja na viongozi wao.

Mfalme wa kwanza ambaye Mungu aliwapa wana wa Israeli alikuwa ni Sauli, ambaye Samweli alimiminia mafuta kwenye kichwa (1 Samweli 9), na kwa huzuni nyingi, Sauli alitambulikana kwa kutokutii kwake; naye hakuwa na moyo wa kuyatenda mapenzi yake Mungu. Baada ya miaka kadhaa, ilimbidi Samweli kumwambia Sauli kwamba Mungu alikuwa amemkataa yeye kuwa mfalme wa Israeli. (Sura 15) na kama tutakavyotambua katika maandiko yote ya ufalme, Mungu bado alikuwa na Nabii-Kuhani katika nyakati hizi za ufalme. Na kama mfalme hakuyatenda mapenzi yake Mungu, Nabii-Kuhani angalimwendea na kumkabili na neno lake Mungu. Kwa dhati, angelisema maneno haya, '*Inakubidi kutenda yale ambayo Mungu anakueleza kutenda, au wewe na watu wote wataadhirika vibaya.'*

Sauli alipokataa kumtii Mungu, Samweli, ambaye alikuwa nayo fursa ya kumchagua mfalme wa kwanza wa Israeli, aliamriwa naye Mungu kumfuta kazi huyu mfalme. Na mahali pake, Mungu alimwongoza Samweli kummiminia mafuta Daudi angali kijana mdogo, na ambaye alikuwa mtu mwenye moyo wenye kumfuata Mungu. (Sura ya 16; na Matendo ya Mitume 13:22) Daudi alikuwa mfalme aliyekuwa bora miongoni mwa wafalme wote wa Israeli. Mungu angelitenda kazi kumpitia yeye, kwa kuwa alimtii. Yeye hakuwa mkamilifu, jinsi sote tunavyofahamu, lakini moyo wake ulikuwa wakati wote ni mnyenyekevu na wenye kujitolea kwake Mungu.

Mfalme wa pili alikuwa ni Sulemani mwanawe Daudi. Hapo mbeleni, Sulemani alionekana kama mtu ambaye Mungu angaliweza kumtumia. Yeye alimwomba Mungu hekima ili kuwaongoza watu wake kwa haki, na Mungu akamkabidhi yeye hiyo Hekima pamoja na utajiri na heshima (1

Wafalme 3:5-14). Sulemani akalijenga Hekalu lake Bwana ambalo babake alikuwa amelikusudia kulijenga (Tazama 1 Mambo ya Nyakati 22).

Sulemani kwa kusudi mbaya akajisalimisha kuzifuata tamaa zake, kwa kuwaoa wanawake mia saba na kuwaweka masuria mia tatu! Hawa wanawake walikuwa ni waabudu sanamu, naye Sulemani akaungana nao katika ibada zao za miungu. (1 Wafalme 11:1-8) Dhambi yake Daudi ilikuwa ni dhambi kuu mno, kama tutakavyoona. Lakini hata hivyo, ni dhambi yake Sulemani ambayo iliyoleta janga kuu na kuvurungika kwingi kwa taifa teule. Rehoboamu mwanawe Sulemani alimfuata Sulemani kama mfalme wa nne wa Israeli (11:9-13).

Baada yake Sulemani, Israeli iligawanyika sehemu mbili. Makabila kumi waligawanyika upande wa kaskazini na kujiita Israeli. Na makabila mawili yakabaki kusini (Yuda na Benyamini), na kujiita Yuda. Wengi wa wafalme wanatajwa katika vitabu vya historia vya Wafalme wa Kwanza na wa Pili na katika Mambo ya Nyakati. Ufalme wa kaskazini haukuwa na mfalme mwema hata mmoja. Watu wa Ashuru (*Syria)* wakatili waliivamia taifa la kaskazini la Israeli na kuyateka makabila yale kumi. Na wao hawakusikika tena. Nalo taifa la Yuda baadaye lilichukuliwa mateka hadi Babeli ambako waliishi kwa miaka sabini. Wakati nchi ya Uajemi *(Persia*) walipoteka Babeli, Mungu alimwongoza huyu mfalme mpya, jina lake Koreshi Mkuu, kuitoa amri kwamba Myahudi ye yote aliyetaka kurudi katika nchi yake na kulijenga Hekalu lake Bwana alikuwa huru. (Tazama 2 Mambo ya Nyakati 36:22-23; Ezra 1).

Maandiko ya ufalme katika vitabu vya historia yaweza kumvuruga ye yote yule, na yanahitaji watu waliokomaa kuyasoma. Lakini unaweza kuwa na mtazamo wenye ulinganifu kihistoria ikiwa utatilia maanani kweli saba za msingi kuhusu historia ya Waebrania.

1. Ufalme mmoja chini ya (Sauli, Daudi, na Sulemani).
2. Ufalme uliogawanyika.
3. Utekwaji wa taifa la kaskazini: Israeli.
4. Kupotea kabisa kwa taifa la kaskazini.
5. Utekwaji wa taifa la kusini na Babeli – Taifa la Yuda.
6. Utekwaji wa taifa la Babeli na taifa la Milki ya Uajemi.
7. Kurudi kutoka nchi ya Babeli (Uajemi) utumwani.

Kwa kujumuisha yote, Ufalme wake Mungu ulikuwa dhahiri wala siyo fumbo. Hii ilikuwa ni milki ya kihistoria na kijiografia ambapo Mungu alikuwa ndiye Mfalme mkuu, na ambapo Mungu mwenyewe alitaka kuwa ni kiongozi wa kipekee mahali dhahiri na panapotambulikana wakati utambulikanao katika historia. Nao watu, wakamkataa Mungu kuwa mfalme wao na badala yake wakamtaka mfalme aliye mwanadamu, na ambaye walimpata. Na matokeo yake yalikuwa ni ya kuhuzunisha mno.

Palikuwapo na mwanamke mmoja mstaarabu ambaye hakuwahi kuisoma Biblia hapo mbeleni. Alikuwa ni mwenye ustarabu, na kitmadumi, naye aliyasema haya kuhusu sehemu hii ya maandiko, *'Sijawahi kusoma cho chote kiovu namna hii katika maisha yangu. Na kama siyo kwa sababu yake Roho Mtakatifu, singeliweza kuvipitia vitabu hivi. Hili ni jambo lisilo nzuri!'* Naam, na kwa hakika huu ni ukweli mtupu! Hebu kumbuka kwamba Mungu hakuwataka watu wake kuwa na wafalme hawa au kuwepo na matokeo yaliyotokea kwa kuwa naye wafalme. Bwana hakuwajibika kwa wao kuwa nao wafalme. Bwana hakuwajibika kwa yale yote ambayo tunasoma katika maandiko ya vitabu vya ufalme – wafalme ndio ambao waliowajibika kwa yote yaliyotokea, kwa kuwa wao walikuwa waovu. Nao watu walikuwa na wajibu kwa kuwa wao ndio waliowachagua hao wafalme. Usisahau haya unapovisoma hivi vitabu vya ufalme.

Ufalme Wake Mungu Katika Agano Jipya

Vitabu vya Maandiko ya ufalme vinatupatia mtazamo unaotusaidia kuelewa dhana kuhusu Ufalme Wa Mungu katika Agano Jipya. Katika historia, wakati Wayahudi waliporudi katika nchi yao ili kuujenga mji pamoja na Hekalu lao lililokuwa limeharibiwa, walitumia ujuzi wao wa takribani miaka mia nne kuanzia Nehemia na baada kifo chake nabii Malaki. Mungu hakuzungumza nao katika hali ya ufunuo hadi wakati wa Agano Jipya.

Ni hadi wakati Wayahudi walipotekwa kwa mara nyingine. Ni kwa wakati huu watekaji wao walikuwa ni Warumi. Sura hiyo ya historia ya Waebrania ilianza wakati Yohana Mbatizaji pamoja na Yesu Kristo Masihi walipovunja kimya cha miaka mia nne kwa kuhubiri ujumbe wa Mungu. Je, ujumbe wao ulikuwa upi? Ulikuwa ni Habari Njema ya Ufalme Wake Mungu!

Yesu mwenyewe aliwaeleza kwamba yeye hakuwa akihubiri kuhusu ufalme wa kihistoria, kitaifa au wa kijiografia. Hii ni kwa sababu watu walikuwa tayari wamekataa jambo hilo zamani zilizopita. Bali, yeye alitaka kuwafahamisha kwamba Mungu alikuwa na nia ya kuwa mfalme wao kwa

mara ya pili; lakini wakati huu kwa mtu binafsi. Na kwa wakati huu, ufalme ungelikuwa ndani mwao (Luka 17:20-21). Je, anafahamu maana yake ni nini? Mwanamume ye yote, au mwanamke, kijana wa kiume au wa kike ambaye atajisalimisha chini ya amri yake Mungu na kumwambia Mungu aipeperushe bendera yake moyoni mwake, kwa kuungama hivi: *'Nakutaka wewe uwe Mfalme wangu, nami nitaka kuwa chini ya utawala wako,'* yeye ameingia tayari katika Ufalme Wake Mungu!

Yesu alizungumza na Rabi au mwalimu kwa jina Nikodemu na kumwambia kwamba asipozaliwa kwa mara ya pili, hangeliweza kuona ufalme wake Mungu. Kulingana na Yesu, hakika unaweza kuwa na macho ya kuona kwamba Mungu ataka kuwa mfalme wako (Yohana 3:3-5; 1 Wakorintho 12:3), na punde uonapo ule ufalme, unaweza kuingia ndani yake. Sisi huyasikia mengi kuhusu kuzaliwa kwa mara ya pili, na mengi yake ni ya kweli. Lakini katika kifungu hicho, somo kuu sio kuhusu kuzaliwa upya, bali ni Ufalme wake Mungu. Kuzaliwa Upya sio mwisho wa mambo yote bali ni njia ya kufikia lengo kuu – na lengo hilo ni Ufalme wake Mungu.

Je, unaweza kukumbuka taratibu ya dhamana katika Mahubiri ya mlimani? Je, alisema lipi kuhusu jambo la muhimu zaidi katika maisha yetu? Tuutafute kwanza Ufalme wake Mungu: *'Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.'* (Mathayo 6:33).

Kutengemea na jinsi ambavyo wewe unavyotumia wakati, mali na uwezo wako, je, ni lipii yenye umuhimu mkuu? Kusudi la kuzaliwa kwa mara ya pili ni kutuleta sisi katika ufalme wake Mungu, ambapo Mungu huyatawala maisha yetu. Mtazamo wa thamani zetu unafanana na shabaha lililo na duara nyekundu katikati mwake pamoja na duara kumi kulizungukia. Kulingana na Yesu Kristo, ufalme wake Mungu na yale ambayo anakuonyesha wewe yahitajika kufananishwa na duara zilizopo kwenye shabaha nyekundu pamoja na zile zenye kulizungukia. Tunahitajika kumtambua na kumtumikia Yeye kama Mfalme wetu, nazo thamani zetu zitadhihirisha kwa ukweli jinsi ambavyo tunafanya hivyo. Maombi yetu yanahitajika kudhihirisha yale ambayo Yesu aliyotufundisha sisi: *'Baba yetu, aliye mbinguni, Jina lako litukuzwe. Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu…'* (Mathayo 6:9-11).

Unaweza kutambua kwamba kabla yake Yesu kutuambia sisi kuomba, 'Utupe,' kwa mara tatu alituambia kumpe Mungu nafasi ya kwanza. Hili ndilo la thamani kuu katika thamani zangu zote.' Na ni baada tu ya hili, ndipo tunaweza kuomba, 'Utupe sisi.' Mambo yanaweza kwenda kulingana na mapenzi yetu, kulingana na jinsi ambayo yalitendeka kwa wana wa Israeli; lakini kama ni muhimu

kwetu, ni lazima nasi tuwe tayari kula chakula katika karamu ya majuto na matokeo yake yajao na kujitakia yetu binafsi, na yaliyo mema machoni petu.

Hili ni jambo ambalo tunatakikana kuliweka maanani tunapojifunza kuhusu ufalme wake Mungu katika maandiko ya Kihistoria ya vitabu vya Wafalme. Na kama utaelewa dhana hii ilioyo katika Agano la Kale, italipuka kwako kama ufunuo wakati utakapoifikiria! Kumbuka kwamba, kusudi la kuzaliwa kwa mara ya pili ni kuuona na kuingia ndani ya ufalme wake Mungu. Je, umeuona ufalme wake Mungu? Na je, umeingia ndani ya ufalme huo? Je, umezaliwa mara ya pili?

SURA YA NANE.

Kusikika Kwake Mungu

Jinsi tulivyotambua katika sura iliyopita, ufalme wake Mungu ni dhana yenye umuhimu sana inayohitajika kutiliwa maanani tunapojifunza maandiko yaliyomo katika vitabu vya Historia vya Agano la Kale. Sehemu nyingine yenye umuhimu katika vitabu hivi ni mifano na maonyo ambayo yamo ndani mwake. Jinsi mtume Paulo alivyoandika: *'Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miiishio ya zamani.'* (1 Wakorintho 10:11). Tutaona mifano mingi na maonyo katika kitabu kilicho mbele yetu.

Samweli wa Kwanza na wa Pili vinatambulika kama kitabu kimoja tangu zamani, jinsi ilivyo kwa kwa Wafalme wa Kwanza na wa Pili pamoja na kitabu cha Mambo ya Nyakati wa Kwanza na wa Pili. Vitabu vya Samweli huzungumzia kuhusu ukweli wake Mungu kwa njia ya hadithi fupi kuhusu watu, na hasa watu watatu. Sura za kwanza nane za Samweli wa kwanza zinatupatia mifano bora ya kuigwa katika maisha na uongozi wake nabii Samweli. Katika sura ya tisa hadi ya kumi na tano, mtazamo unamgeukia mfalme wa kwanza wa Israeli, Sauli ambaye maisha yake ni onyo kuu kwetu sote. Kuanzia Samweli wa Kwanza sura ya kumi na sita na kuendelea hadi mwisho wa Samweli wa Pili (sura thelathini zote), anayetajwa zaidi ni Daudi. Daudi ndiye mfalme bora kuwahi kuitawala nchi ya Israeli, na ukilinganisha na nafasi ile Roho Mtakatifu anampa katika hadithi yake, hakika yeye ni mmoja wa watu muhimu sana katika Biblia.

Pamoja na nafasi iliotengwa kwa ajili yake katika kitabu cha Samweli, Daudi pia aliandika zaidi ya nusu ya Zaburi. Nyingi ya Zaburi hizo ni zina utangulizi wenye maelezo mafupi kuhusu matukio yaliyokuwa wakati alipoziandika Zaburi zile. Tunaweza kupata ufahamu mkubwa zaidi kwa kusoma zaburi zake na kufahamu juu ya maisha yake katika Samweli wa Kwanza na wa Pili. Pia, tunaweza kupata mwangaza zaidi kuhusu maisha na hisia zake katika vitabu vya Samweli kutoka Zaburi alizoandika kuhusu ujuzi wake ambazo zimeandikwa katika vitabu hivyo viwili vya historia.

Hivyo basi, watu watatu ambao tunahitaji kuwatazama katika ukachambuzi wetu wa Samweli wa Kwanza na wa Pili ni Samweli, Sauli, na Daudi. Hebu tuanze na Samweli.

Samweli

Jina Samweli linatokana na maneno mawili katika lugha ya Kiyahudi yanayosema, 'kusikia' na 'kutoka kwa Mungu.' Jambo hili lanakubalika hasa tunapotambua jinsi yeye alivyozaliwa. Mama yake Hana aliishi siku nyingi kwa kuugua na kusikitika kwa kuwa alikuwa tasa. Nyakati hizo, kumzaa mwana ilikuwa ni ishara ya baraka zake Mungu, na kwa sababu hiyo, Hana alikuwa na wazo kwamba utasa wake ulimaanisha kwamba Mungu alikuwa hapendenzwi naye.

Siku moja, wakati jamaa yake walipokuwa wakila na kunywa katika hema lililokuwa huko Shilo, yeye alilia kwa uchungu mwingi na kumwomba Mungu ampe mtoto. Aliomba kwa moyo wake, huku midomo yake ikionekana kama anena, sauti yake isisikiwe; kwa hiyo huyo kuhani Eli aliyekuwa ni mzee alimdhania kuwa amelewa! Ndipo Eli akamwambia, *'Je! Utakuwa mlevi hata lini? Achilia mbali divai yako.'* (1 Samweli 1:14) Wakati Hana alipomweleza hali yake, Eli alisikitika sana na kumpa baraka na kusema kwamba Mungu amjalie haja yake aliyomwomba (15-17). Naye Mungu alitenda hivyo. Elkana ndipo akamjua mkewe Hana; naye Bwana akamkumbuka. Ikiwa wakati ulipowadia, Hana akachukua mimba na kuzaa mtoto mwanaume; akamwita jina lake Samweli, akisema, Kwa kuwa nimemwomba kwa Bwana. (20). (ni vyema kufahamu kwamba wakati jina lo lote lamalizikiapo kwa herufi 'eli', huwa na uhusiano naye Mungu. Kama, Danieli, kwa kuwa katika lugha ya Kiyahudi, ELI humaanisha Mungu.)

Baada yake Samweli kuachishwa maziwa, mama yake Hanna alimpeleka kwenye nyumba ya Bwana, kwa kumpa Kuhani Eli. Jina lake liliambatana na mahali hapo kwa kuwa wakati Samweli akiwa mdogo akilewa naye Eli, katika uwepo wake Mungu Samweli aliisikia sauti yake Bwana (Sura

ya 3). Huzuni ni kwamba ujumbe ule ulikuwa ukimkemea Eli kwa kuwa yeye hakuwaadhibu wala kuwakanya wanawe, kwa kuwa hawakumjali Bwana wala haki ya makuhaniilivyokuwa kwa watu (Tazama 2:12-17, 22-25, 27-36). Samweli, aliyemtazama Eli kama baba mzazi, ilimbidi kumwambia huyu kuhani mzee kwamba angalitolewa katika ukuhani.

Jina 'Kusikia kutoka kwa Mungu' lilimfaa Samweli alipokomaa na kuwa mtu mzima. Maandiko yanasema kwamba kutoka sehemu za kaskazini hadi kwa ncha ya kusini ('kutoka Dani hadi Beer-sheba'), Israeli yote ilitambua kwamba Samweli amewekwa kuwa nabii wa Bwana (3:19). Israeli wote walilisikia neno lake Mungu kupitia huyu mtu. Hivyo basi, 'kusikia kutoka kwake Mungu' ni jina linalomfaa sana huyu Samweli.

Maisha yake Samweli yanatushirikisha katika mifano kadhaa ya kuigwa. Kwanza, Yeye na mama yake wanatuonyesha malezi ya Kiungu pamoja na elimu. Ili tuwe na uwezo pamoja na Uungu, tunahitaji kutilia maanani sehemu yetu kama wazazi kuwa ni ya kuwajibika na kutoka kwake Mungu. Na ni lazima tutilie maanani kwamba watoto wetu ni baraka kutoka kwake Mungu. (Zaburi 127:3). Wakati tunapokiri na kuipokea hii thamani kuu kama Samweli, na baadaye Yohana Mbatizaji, wana wetu watakuwa na baraka pamoja na malezi ya kiroho.

Jambo la pili, Samweli alikuwa ni mfano mkubwa kuhusu yale ambayo yanatokana na malezi ya Kiungu tunapomwona akiongoza Israeli kutoka kwa giza ya kiroho, inayojulikana kama 'Siku Waamuzi walipotawala.' Baadhi ya wasomi wanamtambua Samweli kama Mwamuzi wa mwisho, na hivyo basi maisha yake yalikuwa sawa na kinara cha ishara katika historia ya Wayahudi.

Tunaliona jambo lingine la tatu ambalo lahitajika kuigwa katika vitabu hivi vya Samweli. Tunamwona huyu mtu mkuu akifanyika na kuwa kiongozi mkuu wa kisiasa, akiunganisha nyakati zao waamuzi pamoja na zile za wafalme. Yeye ndiye aliyewatia matufa Sauli pamoja na Daudi aliyekuwa kiongozi mkuu wa Israeli. Wakati wa dhiki kuu, kama misuko-suko ya nyakati za uongozi wake Sauli, Samweli aliendelea kuwa mwaminifu kwake Bwana na wana wa Israeli hadi mwisho wa maisha yake.

Sauli

Pale maisha yake Sauli yanapotupa shauku kuu ya kuuiga mfano wake ni wakati maisha yake yafanyika kuwa maonyo ya kuhuzunisha.

Sauli ni mtu mwenye ubishi mkuu katika maandiko, kwa kuwa maisha yake ni ubishi mkuu wa kithiolojia: Je, mtu anaweza kukombolewa siku ya leo na kupotea siku ya kesho? Wengi husema kwamba, jambo hilo haliwezekani, huwezi kupoteza wokovu na kwa sababu hiyo kuyakariri maandiko mengi wakitetea kwamba wakati wote wana wapotevu hurudi nyumbani. Hali wengine husema kwamba inawezekana, waweza kupoteza wokovu; huku wakitumia mfano wake Sauli. Maandiko mengi yanaonyesha kwamba unawaweza kupoteza wokovu wako. Sauli aonekana alikuwa na ushuhuda wa kweli katika wokovu wake na pia inaonekana kwamba aliupoteza wokovu ule wa kimiujiza katika maisha yake. Wale ambao wanaitetea dhana hii husema kwamba inakubidi kuzaliwa mara nyingine kila wakati unapokuwa mpotevu.

Naamini kwamba Biblia inatufundisha kwamba Mungu hututeuwa na kutuokoa kwa neema na mapenzi yake mwenyewe. Hivyo basi, ikiwa mtu ana ushuhuda na wokovu wa kweli–na ikiwa kwa hakika amezaliwa kwa mara ya pili–yeye hawezi kuupoteza wokovu wake.

Sauli alikuwa na ushuhuda wa kiroho na hapo mwanzoni alionekana kwamba alikuwa ni mtu wa kiroho. Baada yake Samweli kumtia mafuta, Mungu alimbadilisha moyo wake (10:9). Sauli alitoa unabii pamoja na kundi la manabii wakati Roho ya Mungu ilipomjia kwa nguvu (10:10-11). Hata hivyo, ni wazi kabisa tunapoendelea kusoma maisha yake Sauli, alikipoteza nguvu hizo za kiroho.

Samweli wa kwanza 9 inatutambulisha kwake Sauli. Jambo la kwanza tunalofahamu kuhusu huyu Sauli ilikuwa kwamba yeye ni mrefu kuliko watu wote katika nchi ya Israeli na mtu mzuri sana (9:2). Umbo lake mtu halistahili kuwa kipimo chetu kuwahukumu wale wengine au sababu ya kuwadhamini wao kwa uongozi. Na kwa upande mwingine, Bwana baadaye alimwaambia Samweli wakati alipokuwa akimtia Daudi mafuta: *'Usimtazame uso wake, wala urefu wa kimo chake . . . Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo.'* (16:7).

Tunapokutana na Sauli kwa mara ya kwanza, yeye na mtumishi wake walikuwa wakiwatafuta punda wa baba yake bila ya mafanikio. Huku wakiwa katika hali ya kukata tamaa, mtumwa wake Sauli alikumbuka kwamba nabii (Samweli) alikuwepo hapo karibu. Na hivyo basi, wao wamwendea huyu mtu wa Mungu, ambapo kwa njia ya kimiujiza Mungu alikuwa tayari amemwandaa Samweli kwa kuja kwao (9:3-14, 18-20). *'Basi Bwana alikuwa amemfunulia Samweli, siku moja kabla ya Sauli*

*hajamwendea, akisema, Kesho, wakati kama huu, nitakuletea mtu kutoka nchi ya Benyamini, nawe mtie mafuta ili awe mkuu wa watu wangu Israeli..' (*9:15-16). Hivyo basi, wakati Sauli anapokutana naye Samweli, yeye alikumbana na mshangao mkubwa mno.

Samweli aliwaalika katika karamu, na kuwaambia kwamba wale punda walikuwa wamepatikana, na kumfahamisha kwamba yeye alikuwa ndiye mfalme ambaye Israeli walimtarajia! (9:21) Kwa mshangao mkubwa, Sauli akajibu akasema, *Je! Mimi si Mbenyamini, mtu wa kabila iliyo ndogo kuliko kabila zote za Israeli? Na jamaa yangu nayo si ndogo kuliko jamaa zote za kabila ya Benyamini? Kwa nini basi, kuniambia hivyo?*

Sauli aongeza sauti yake kwa sauti zingine ambazo tayari tumezisikia katika Agano la Kale wakati Mungu alipomwita kiongozi. Gideoni alisema maneno haya haya wakati Mungu alipomwita yeye kuwa mkombozi mkuu. Na kama unaweza kukumbuka, mwishoni mwa Waamuzi, kabila la Benyamini lilikuwa karibu kuangamizwa baada ya waume wa huko Gibea kumjua na kumtenda uovu suria wake Mlawi mmoja katika hadithi ya kushangaza inayo katika Maandiko (Tazama Waamuzi 19-25). Ni wanaume mia sita peke yao waliobaki baada ya Israeli kuifanya vita vya wao kwa wao, na iliwabidi kutafutiwa wake ili kabila hiyo lisipotee kutoka katika uso wa nchi (Waamuzi 21).

Huu ulikuwa ndiyo urithi wake Sauli. Sio ajabu kwamba alisema yeye alizaliwa katika kabila lililo ndogo na jamii iliyokuwa ndogo kabisa. Unyenyekevu wake ulikuwa wa kweli na dhahiri kabisa. Hata hivyo, Samweli akala pamoja naye Sauli na kumtia mafuta ili awe mfalme siku iliofuatia, kulingana na mapenzi yake Mungu. (1Samweli 9:22-10:1).

Sauli hakuwa ni mfalme mwema. Yeye angalifanyika kuwa mfalme mkuu na mtu wa kiroho. Mungu alimpangia kumfanya yeye pamoja na wanawe wafalme katika Israeli milele. Lakini kwa sababu ya kutokutii kwake, ufalme ulinyakuliwa kutoka kwake. (13:13-14).

Ni jambo gani ambalo lilitokeas kwake mtu ambaye Mungu alikuwa ameubadilisha moyo wake? Wakati moja alikuwa ni mtu mdogo machoni pake (15:17), lakini kwa wakati huu alionekana kufikiria kwamba mawazo yake yalikuwa ni mhimu kuliko yake Mungu. Yeye alikataa kumtii Mungu mara mbili. Kwanza, katika vita pamoja nao Wafilisti, yeye alishikwa na hamaki wakati Samweli alipochelewa kuitoa dhabihu, hivyo basi kuuchukuwa wadhfa wake kuhani na kuitoa ile kafara yeye mwenyewe (Sura ya 13).

Wakati Samweli alipomkemea, pia aliutabiri uongozi mkuu wake Daudi kama mfalme mkuu kuwahi kuwepo Israeli. Samweli alitabiri kwamba Mungu angalimpa Ufalme Wake mtu aupendezaye moyo wake, naye amemwamuru yeye kuwa mkuu juu yta watu wake, kwa sababu Sauli hakulishika neno lile Bwana alilomwamuru. (13:14) Hapa ndipo tunamsikia Daudi kwa mara ya kwanza.

La pili, Sauli aliharibu fursa ya pili ambayo Mungu aliyompa kwa kukataa kuwaangamiza Amaleki (Sura 15). Sauli alikuwa ameamrishwa kuharibu kila kitu – watu wote, fahali wote, kondoo wote, ngamia wote, pamoja na punda. Kila kitu! Lakini akiwa pamoja na Jeshi lake wakanyakua mabaki ya utekaji wao hata kumweka hai mfalme wa Amaleki. Naye Bwana Akamwaambia Samweli, *'Najuta kwa sababu nimemtawaza Sauli awe mfalme; maana amerudi nyuma, asinifuate, wala hakufanya nilivyomwamuru…!'* (15:11).

Huku akiwa amesikitika, Samweli alikabiliana naye Sauli, ambaye alidai kwamba aliyatii maagizo yake Bwana kikamilifu, hata baada yao kukisikia kilio cha kondoo kilicho sikika kwa mbali (13-14). Kisha Sauli akaitoa sababu kwamba mabaki yao wanyama hawa yalikuwa ni ya kumtolea dhabihu Mungu. Lakini Samweli hakuyaamini maneno hayo. Baadala yake, alimwaambia Sauli, *'Je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu sawasawa na kuitii sauti ya Bwana? Angalia kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia kuliko mafuta ya beberu. Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi, na ukaidi ni kama ukafiri na vinyango...'* Wakati Samweli alipojaribu kuondoka pale, Sauli aliushika upindo wa vazi kale, nalo likararuka. Samweli akamwambia Sauli kwamba Bwana ameurarua ufalme wa Israeli, naye amempa jirani yake, aliye mwema kuliko yeye. (15:22-29).

Hapo baadaye, tunaona kwamba Roho wake Mungu alimwacha Sauli (18:17). Hali hii inaitwa 'Ikabodi, maanake, 'Utukufu umeondoka.' Nyakati za Agano La Kale Roho yake Mungu aliwajia watu, na kama wao hawakumtii yeye, Roho aliwaacha. Siku ya leo tuna ahadi yake Kristo aliyefufuka kwamba kama Yeye akiishi ndani mwetu, Yeye hatatuacha kabisa wala kutupungukia. Waebrania 13:5). Lakini hata hivyo, maisha yake Sauli ni onyo kwetu la kututikisa. Ingawaje Yeye hatatuacha sisi siku ya leo, sisi tunaweza kumwacha yeye, kumhuzunisha au kumzima. Maisha yake Sauli ni onyo kinyume cha kutokutii kwa wenye kutiwa mafuta–onyo kuhusu kutumia vibaya neema na baraka yake Mungu.

SURA YA TISA.

Utiifu Uliotiwa Mafuta

Tunapozidi kukagua maisha ya Sauli na Daudi, tunahitajika kukumbuka kwamba upako wake Roho Mtakatifu hauwafanyi watu kuwa mashine au gogo. Bado tuna uchaguzi huru. Katika hali yake Sauli, yeye alikuwa na fursa ya kufanya uchaguzi, na kwa huzuni, kila mara anapofanya uchaguzi uliokuwa mbovu. Na kwa sababu hiyo, Bwana akamwondoa Roho wake kwake (1 Samweli 16:14; 18;12).

Je, yale yaliyotendeka kwake Sauli yanaweza kutendeka siku ya leo? Naamini kwamba Roho Mtakatifu alihusika kwa njia tofauti na watu nyakati hizo za Agano la Kale kuliko anavyohusika nasi siku ya leo, kwa sababu ya msalaba na Pentekote. Tunamsikia Daudi akiomba, *'Usinitenge na uso wako, wala roho yako iliyotulia ndani yangu.'* (Zaburi 51:11). Yesu sasa anatuambia hivi, *'Sitakuacha kabisa wala kukupungukia wewe.'* (Waebrania 13:5). Tunapoupata ushuhuda huo wa uzao upya, Mungu huanza kazi yake ya kiroho ndani mwetu na kuitenda '*. . . . hata siku ya Yesu Kristo'* (Wafilipi 1:6; 2:13). Katika siku hizi zetu, kazi yake Roho Mtakatifu ina mitazamo miwili: (1) Kazi yake ndani yetu, ambayo ni kuzaliwa upya, na mtazamo huu wa kazi yake unadhihirishwa kama tunda la Roho. (Wagalatia 5:22-23). (2) Baraka yake au upako wake juu yetu. Huu ni mtazamo wa kazi Yake unaodhihirishwa kupitia vipawa au karama za Roho Mtakatifu, ambazo zinatuwezesha kwa huduma mbali mbali.

Lakusikitisha zaidi ni kwamba, kutokutii kwake Sauli kulimfanya Mungu kumtupilia mbali na uwepo wake na kumwondoa Roho Mtakatifu kwake. Jambo hili lilipotokea, maisha yake Sauli yalifanyika kuwa ishara wazi ya yale tunayotaja kama kuvurungika kwa utu.

Sauli Avurungika.

Katika siku ya leo, tungemwita 'mtu aliyechanganyikiwa na mwenye kichaa.' Kamusi inaelezea neno la mwisho kama 'utu wenye kuchanganyika.' Maelezo haya yanasema kabisa jinsi hali yake Sauli ilivyokuwa. Sauli alipatwa na kichaa. Hivi kwamba yeye alikuwa na hofu kuwa kila mtu alikuwa akimvizia kwa nia ya kumfanyia hila kinyume chake, na hasa Daudi. Hapo baadaye, anashikwa na wivu mwingi juu ya Daudi, huku akiwa amejishawishi kwamba Daudi amenuia kuchukua ufalme kutoka kwake. (Samweli 18:8; 20:30-31). Na kwa njia fulani, labda huyu Sauli

aliteseka kutokana na unabii wake Samweli kuhusu kupokonywa ufalme wake na kupewa mtu aliye bora–mtu ambaye angeliyatenda mapenzi yote yake Mungu kwa moyo wake wote. (13:14).

Tabia kuu iliyotawala maisha yake Sauli ilikuwa ni kutokutii. Neno moja ambalo Mungu aliliandika juu ya maisha yake huyu Sauli ni, 'Ikabodi' maanake, 'Utukufu umeondoka.'

Daudi

Mtu Mwenye Kufuata Moyo Wake Mungu

Maisha yake Daudi yalikuwa kinyume kabisa na huyu Sauli. Tabia kuu katika maisha yake huyu Daudi ilikuwa ni Utiifu–Alikuwa mtu mwenye kufuata moyo wake Mungu ambaye angalitimiza mapenzi yote yake Mungu. Pale ambapo maisha yake Sauli yalipovurugika kwa kujipatia talaka kutoka kwake Mungu. Mungu alikuwa akiyaleta mambo yote pamoja kwake Daudi kwa kuwa Daudi alitilia maanani utiifu kuliko Sauli ambaye alitilia maanani zaidi kutokutii.

Mungu alimtuma Samweli katika nyumba yake Yese wa Bethlehemu, ili kumtia mafuta yeye ambaye angechukuwa uongozi na kuwa mfalme baada yake Sauli. Lakini huyu nabii-kuhani alifikiria kwamba umbo la kuvutia ya mwana wa kwanza katika nyumba yake Yese ilionekana kwamba ni bora kwa mfalme atakayefuata. Hivyo basi, ilimbidi Mungu kuurekebisha mtazamo wake kwa ukweli huu mkuu: *'Usimtazame uso wake, wala urefu wa kimi chake; kwa maana mimi nimemkataa. Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo!* (16:7).

Yese akawapitisha wanawe wote saba wenye nguvu mbele yake Samweli, lakini Bwana hakumchagua ye yote kati yao. Labda Samweli akipigwa na bwutaa, akamwuliza Yese, kama alikuwepo mwana mwingine kando yao hawa waliokuwepo mbele zake. (16:10). Naam, yeye alikuwa naye aliyebakia–Daudi–mwanawe mdogo aliyekuwa akiwachunga kondoo wake (11). Samweli akamwambia Yese amlete mara moja, na hivyo basi huyu Daudi aliyekuwa mchanga zaidi na mdogo kuwaliko nduguze, (Jambo hili walikumbuka?) alikuwa ndiye aliyeteuliwa kuwa mfalme baada yake Sauli. (12) Na hapa Samweli akamtia mafuta, na roho wa Bwana ikamjia Daudi kwa nguvu tangu siku ile. (13).

Hata hivyo, ilichukuwa wakati mrefu kufikia wakati ambapo Daudi angefanyika kuwa mfalme. Katika sehemu kubwa ya kitabu cha Samweli wa Kwanza, tunamwona Daudi katika taasisi yake Mungu akijitayarisha. Huku Sauli akijawa nao wivu mkuu na uuaji akimtafuta, Daudi aliyapitia majaribu ya kila aina ambayo yalimfundisha kumtumainia na kumtii Mungu bila kujali mazingira yake. Ujuzi wote alioupata ulimfanya kuwa tayari kwa makusudio ya Mungu katika maisha yake. Je, unafahamu kwamba Mungu hulitenda jambo hili kwetu pia? Kila siku tunayoishi, yeye hututayarisha kwa siku inayofuatia. Ikiwa tunampenda Mungu na tumeitwa kulingana na kusudi lake, yote yale tunayopitia husaidia katika yale Mungu angelipenda tufanye katika siku za usoni (Tazama Warumi 8:28).

Hebu tutazame baadhi ya matukio ambayo Mungu alimpitishia Daudi kisha tuangalie jinsi alivyofumwa na kuwa mtu aliyemtarajia kuwa.

Daudi Akiwa Mchungaji Kondeni

Wengi miongoni mwa viongozi walio katika Biblia, kama vile Musa na Daudi, walikuwa wachungaji wa kondeni. Kuna sababu ya jambo hili, nao ujuzi wake Daudi unadhihirisha sababu hii. Katika matukio kadha huku Daudi akiwachunga mifugo wa babake, ilimbidi kupigana na Simba pamoja na Dubu ambao waliwavamia kondoo. (1 Samweli 17:34-36). Na Kama alivyokuwa Yesu Masihi, Daudi pia alikuwa tayari kutoa maisha yake kwa ajili ya Kondoo wake. (Hebu linganisha Yohana 10:11-15). Ni dhahiri kuwa Mungu alikuwa ameliona jambo hili na kufikiria, *'Ikiwa huyu kijana anahisi hivi kuhusu kondoo wa baba yake, ni lazima kwamba atajihisi vivyo hivyo kwa ajili ya kondoo wangu. Nitamfanya yeye awe mfalme!'*

Daudi Mwimbaji

Sauli akiwa katika wingu kuu la kujikunyata chini ya huzuni na moyo wenye kuvunjika. Kwa hakika alihitaji usaidizi. Nao watumishi wake walimshauri kusikiza nyimbo za kinubi na kuponya roho ile mbaya, naye mmoja wao akasimulia sifa zake Daudi, kwamba alikuwa kijana mwenye umbo la kupendeza, mwanawe Yese kutoka mji wa Bethlehemu. Alikuwa stadi wa kupiga kinubi, tena mtu shujaa, na hodari wa vita, anenaye kwa busara, mtu mzuri, 'La ziada ni lipi,' ambaye Bwana yu pamoja naye. (16:18).

Na kwa sababu hiyo, Daudi akaifariji na kuituliza roho yake Sauli kwa nyimbo (23). Yamkini aliimba zaburi ambazo ameziandika. Kumbuka kwamba, Daudi aliziandika zaidi ya nusu ya zaburi

zilimo katika kitabu cha Zaburi; ambacho ndicho kitabu cha nyimbo za kuabudu katika Israeli. Kuelekea mwishoni wa maisha yake, alitayarisha uongozi wa hekalu pamoja na taratibu ya ibada– iliyowausisha kuhani elfu nne ambao walivicheza vyombo ambavyo Daudi mwenyewe alikuwa ametengeneza. 'Kumsifu Bwana.' (1 Mambo ya Nyakati 23:5) kuliko mtu mwingine ye yote yule katika historia ya watu wake Mungu. Daudi aliunganisha pamoja nyimbo na neno lake Mungu na kuwa sehemu kitu kimoja daima.

Daudi Kiongozi wa Watu

Daudi alifanyika kuwa kiongozi jenerali mkuu na mwenye ushawishi mwingi. Askari jeshi wake walikuwa tayari kusalimisha maisha yao kwa ajili yake. Daudi alipokuwa mkimbizi kutoka kwa Sauli huku akijificha katika mapango ya huko Adulamu, Wafilisti walivamia Israeli na kuteka Bethlehemu. Wakati watatu miongoni mwa askari jeshi wake walioshupavu na hodari walipomtembelea kumwona, yeye alizungumza tu kwa mzaha kwamba aliyatamani mno maji kutoka kisima cha mji wa Bethlehemu. Wao kama mashujaa wake walikubana kwa ujasiri na majeshi ya adui hivi kwamba wakapenya katikati ya ulinzi wao hadi kukifikia kisima cha mji cha Bethlehemu na kumletea Daudi maji hayo anywe! Lakini Daudi hangeliwaza kunywa yale maji–bali aliyamimina mbele za Mungu, huku akisema, kwamba yeye hastahili yale maji kwa kuwa wale askari jeshi wake hodari walihatarisha maisha yao ili kumletea yale maji. (1 Samweli 13-17) Inasemekana kwamba kiongozi ni mtu mwenye wafuasi. Kwa hakika Daudi alikuwa ni kiongozi wa watu.

Daudi Pamoja na Yonathani

Mfano mmoja wa kuvutia zaidi duniani kote unapatikana katika urafiki wake Daudi na mwanaye Sauli, yaani Yonathani. Wakati Daudi alipopata habari kwamba Yonathani ameuawa, yeye alisema, *'Nimesikitika kwa ajili yako, Yonathani, ndugu yangu, ulikuwa ukinipendeza sana; upendo wako kwangu ulikuwa wa ajabu, kupita upendo wa wanawake!* (2 Samweli 1:26).

Waume wengi hawawezi kumtazama mwanamume mwenzao kwa uso na kusema, *'na nakupenda.'* Hii ni kwa sababu wao wanaogopa uhusiano wa kulawiti. Lakini urafiki kati yake mwanamume na mwanamume mwingine au mwanamke na mwanamke mwingine ni jambo la kuvutia sana. Katika hali ya kimaisha, wakati Mungu anapokifuma kitu chenye kuvutia katika maisha haya, Shetani hukivuruga kwa dhambi mbaya ili kutufanya tukitupilie mbali kutokana na kusudio yake Mungu. Ni Mungu aliyeushona pamoja mioyo yao Daudi na Yonathani.

Siri ya maisha yake Daudi ya kiroho ilikuwa ni lipi? Yeye alikuwa mtu aliyejitolea kikamilifu kwa Mungu, na alitaka kutenda mapenzi yake. Daudi adhihirika katika kurasa za maandiko kama mfano mkuu jinsi Mungu anavyoweza kufanya kupitia mtu aliyejitolea kabisa kwake Bwana.

SURA YA KUMI

Jinsi ya Kutokufuzu kwa Njia Bora

Kulingana na maandiko, ufunguo wa kupokea upako wa Roho Mtakatifu ni utiifu. Yesu akasema, *'Mkinipenda, mtazishika amri zangu. Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake.'* (Yohana 14:15,23) Kwa maneno mengine, utiifu ndio takwa la kwanza katika kupokea ujuzi na uwezo wa Roho Mtakatifu (Tazama Matendo 5:32). Na kwa sehemu kubwa ya maisha ya Daudi, yeye alikuwa mfano uliong'aa wa kweli hii.

Kupambazuka Kwa Mafanikio

Mfano bora wake Daudi kuhusu utiifu ulio chini ya upako ulifikia kilele chake katika Samweli wa Pili sura ya saba. Alikuwa na nia ya kumjengea Mungu nyumba katika moyo wake. Yeye mwenyewe aliishi katika nyumba iliyojengwa kwa mierezi na kwa sababu hiyo, alitaka kumjengea Mungu jumba kuu kwa kuwa wakati huo makao yake Mungu yalikuwa hema la mikutano. Hata hivyo, Nathani nabii alimweleza Daudi kwamba Mungu hangelimtaka yeye kumjengea makao, kwa kuwa yeye ndiye angelimjengea Daudi nyumba yake-Urithi wa kifalme, urithi wake wana ambao wangelitawala Israeli, katika ufalme usio na mwisho. Masihi angalitokana katika uzao wake Daudi, na angeimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake haungekuwa na mwisho. (Luka 1:33).

Daudi alikumbana na haya kwa maombi yenye kuvutia mno: *'Mimi ni nani Bwana Mungu, na nyumba yangu ni nini, hata umenileta hata hapa? Tena jambo hili lilikuwa dogo machoni pako, Ee Bwana Mungu; hata umeleta habari ya nyumba yangu mimi, mtumwa wako, kwa miaka mingi inayokuja baadaye; na hayo kwa nama ya kibinadamu, Ee Bwana Mungu. Kwa ajili ya nenoi lako, na kiwa moyo wako mwenyewe, umetenda makuu hayo yote, ili umjulishe mtumwa wako.'*(2 Samweli 7:18-21).

Siyo kwa sababu ya yale tulio nayo wala jinsi tunavyotenda hivi kwamba Mungu atubariki sisi. Kiini hasa cha yale ambayo Daudi aliyoyasema katika maombi yake kilikuwa kwamba, Mungu hutubariki kwa sababu ya Neema Yake.

Wingu la Dhoruba ya Dhambi

Tunapofika katika Samweli wa pili sura ile ya kumi na moja, tunaanza sura nyingine katika maisha yake Daudi–moja wapo ya sura ngumu na ndefu katika maisha yake. Mahali hapa Daudi anaacha kuwa ni mfano mwema na kuwa onyo mojawapo ya zile kuu katika Biblia. Daudi atumbukia katika dhambi ya uzinzi na uuaji na kwa muda wa mwaka mmoja, huku akijaribu kulificha.

Je, inawezekanaje mtu ambaye moyo wake na hoja yake kuu ni katika kumpendeza na kufanya mapenzi yake Mungu kuanguka kwa njia hii ya kushangaza? Yamkini zipo sababu kadhaa ambazo zinatambulikana kuhusu kuanguka kwake Daudi katika dhambi. Jambo la kwanza, Daudi alitenda dhambi kwa kuwa yeye ni mwanadamu. Ingawaje yeye alikuwa ni mtu mwenye kumcha Mungu, alikuwa bado ni mwanadamu na kwa sababu hiyo asingeweza kujipokonya kutoka katika uwezekano wa kutenda dhambi au kushindwa kiroho. (Tazama 1 Wakorintho 10:12,13).

Jambo la pili, mafanikio yake Daudi yalimfanya kuwa kwenye hatari ya janga lo lote lile. Tunasoma katika Samweli wa pili sura ile ya kumi na moja msitari wa kwanza *'Hata ikawa, katika mwanzo wa mwaka mpya, wakati watokapo wafalme kwenda vitani, Daudi akampeleka Yoabu na watumishi wake pamoja naye, na Israeli wote; wakawaanganmiza wana wa Amoni, wakahusuru Raba. Lakini Daudi mwenyewe akakaa Yerusalemu.'*

Wakati ambapo alipapwa kuwaongoza majeshi yake katika vita, Daudi alibakia nyuma Yerusalemu na kumtuma Yaobu badala yake. Daudi alitenda dhambi kwa kuwa yeye hakufanya mapenzi yake Mungu. Inawezekana pia kuwa Daudi alitenda dhambi kwa kuwa alikuwa amefikia kilele cha ufanisi wake. Mtume Paulo alisema haya wakati mmoja, 'Najua kudhiliwa. Tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa.' (Wafilipi 4:12). Kwa hakika hali ya kiroho ya mtu ndio humwezesha kukumbana na hali ya kuwa na mahitaji. Pia, inahitaji uweza mkuu zaidi katika kiroho chake mtu ili kukabiliana na ufanisi zaidi. Wakati sisi tumo katika hali ya ufanisi, tengemeo letu kwake Mungu huwa lengevu mno. Na jambo hili hutufanya, jinsi vile Daudi alivyokuwa katika hadhari nyingi.

Huku jeshi lake Daudi likiuzingira mji wa Raba, huko Yerusalemu; Daudi naye alitembea juu ya dari ya nyumba yake na kumwona mwanamke mrembo sana akioga–naye akamtamani. Na kwa sababu yeye alikuwa mfalme, alikuwa nao uwezo kutwaa kile alichokitaka. Kwa hivyo akamchukua yule mwanamke. Uzinzi wake huyu Daudi haukuwa ni hali ya watu wawili–ni bora kutilia jambo hili maanani unapoendela kusoma. Hii ni kwa kuwa huyu Bath-sheba hakuwa na uwezo katika hili. Siyo jambo ambalo yeye alitaka kulitenda. Mume wake Uria alikuwa mmoja wa watumishi hodari katika jeshi lake Daudi, na jinsi ilivyo; yeye alimpenda mumewe kwa dhati. Lakini mumewe alikuwa mbali akipigana vita vyake Daudi.

Wakati Daudi alipofahamu kwamba huyu Bash-sheba amekuwa mja mzito, alimrudisha nyumbani mumewe kutoka vitani. Daudi alijaribu kumfanya Uria kurudi kwake nyumbani na kulala na mkewe, Bash-shaba, lakini uaminifu wa kujitolea kwake Uria kama askari haungemruhusu kufanya hivyo. Daudi alijaribu kumshawishi Uria kwa kila hali lakini Uria hangekubali kuingia nyumbani kwake na kuwa pamoja na mkewe. Hii ni kwa sababu kama askari jeshi, yeye alifahamu kwamba siyo jambo njema kufurahia wakati askari wenzake walikuwa katika hatari na ungumu wa vita. Kwa sababu hiyo, Daudi akapeleka ujumbe–kwa mikono yake Uria – kwake Jenerali mkuu wa jeshi, Yoabu: *'Akaandika katika waraka huo, kusema, Mwekeni Uria mbele ya watu penye vita vikali, kisha ondokeni, mmwache, ili apigwe akafe.'* (2 Samweli 11:15).

Naye Jenerali Yaobu alituma ujumbe baadaye kwake mfalme, akimpatia ripoti kamili kuhusu hali ya vita akiongezea kusema*: 'Na Uria, Mhiti, mtumishi wako, amekufa naye.'* (24). Uria aliuawa, na kwa hivyo Daudi hakuwa chini ya hukumu ya uzinzi peke yake, bali pia hukumu ya mauaji. Dhambi hii inapochunguzwa mara nyingine katika Mambo ya Nyakati, mauaji yake Uria ndio yaliotiliwa mkazo mkuu kama kina cha dhambi yake Daudi. Naye alikuwa mwenye hatia kwa kuishi maisha ya unafiki yenye uongo. Daudi aliificha dhambi yake kwa muda wa mwaka mzima, huku akifikiria kwamba hakuna mtu aliyeifahamu ila yeye mwenyewe na Jenerali wake Yoabu. Mwaka huo wa kuificha dhambi ulikuwa mojawapo ya miaka yenye usumbufu mwingi katika maisha yake Daudi. (soma Zaburi zake 32 na 52 kuhusu ya moyoni mwake).

Hukumu iliyomkalia Daudi kwa hakika ilimfanya kuwa mgonjwa mwilini mwake. Mwishowe, yeye alimgeukia Mungu*: 'Nalikujulisha dhambi yangu, wala sikuuficha upotovu wangu. Nalisema, Nitayakiri maasi yangu kwa Bwana, Nawe ukanisamehe upotovu wa dhambi yangu.'* Daudi alisema kwamba wenye kumcha Mungu wahitajika kuomba kwa ajili ya baraka ya msamaha. Je, hili

lamaanisha kwamba wamchao Mungu wanaweza kutenda dhambi? Naam, inawezekana. Lakini kuna njia ambayo ukuu wake Daudi unatiliwa mkazo kwa njia ambayo yeye anakumbana na dhambi yake pamoja na matokeo ya dhambi hiyo.

Miale ya Nuru kwenye Anga lenye Giza

Tunaposhindwa, jambo la muhimu ni lile tunalotenda baada ya kushindwa kwetu–jinsi tunavyokumbana na kushindwa kwetu. Na ni katika sehemu hii maishani mwake Daudi, hata baada ya kuitenda dhambi, kunakuwa mfano mkubwa katika Biblia kwa ajili yetu.

Kukabiliana

Katika 2 Samweli 12, nabii jasiri jina lake Nathani alitembelea katika makao yake Daudi. Akaitoa hadithi kuhusu tajiri moja ambaye alikuwa na mifugo wengi na maskini mmoja katika mji huo ambaye alikuwa na mwana kondoo mmoja tu aliyempenda sana. Huyu maskini alimpenda sana huyu mwana kondoo wake; kama mpendwa kwa watoto wake. Huyu mwana kondoo alikula katika posho lake na kukinyewea kikombe chake. Lakini wakati huyu tajiri alipotembelewa na mgeni, yeye hakumchinja mmoja wa wanyama katika mifugo wake, ila alimchinja yule mwana kondoo wa yule maskini na kumfanyia mgeni wake kitoweo.

Daudi alipoisikia hii hadithi, kwa hasira nyingi akasema*, 'Aishivyo Bwana, mtu huyu aliyetenda jambo hili, hakika yake astahili kufa!'*(5). *Kisha Nathani akamwelekezea kidole Daudi na kusema, 'Wewe ndiwe mtu huyo! Bwana Mungu wa Israeli, asema hivi, Nalikutia mafuta, uwe mfalme juu ya Israeli, nikakuokoa na mkono wa Sauli nami nikakupa nyumba ya bwana wako, na wake za bwana wako kifuani mwako; nikakupa nyumba ya Israeli na ya Yuda; na kama hayo yangalikuwa machache, ningalikuongezea mambo kadha wa kadha. Kwa nini umelidharau nene la Bwana, na kufanya yaliyo mabaya machoni pake? Umempiga Uria, Mhiti, kwa upanga wa wana wa Amoni. Basi, sasa, upanga hautaondoka nyumbani mwako, kwa sababu umenidharau, ukamtwaa mkwewe Uria, Mhiti, kuwa mke wako.'* (2 Samweli 12: 7-9).

Machoni pa wote waliokuwa katika makao ya kifalme, Nathani alimkabili Daudi kwa dhambi yake. Kumbuka, Daudi alikuwa mfalme na angalisema, 'kichukuwe kichwa chake huyu.' Lakini hakutenda hivyo. Badala yake, kwa unyenyekevu mwingi akaitubu dhambi yake. (12:13a). Mungu akamsamehe yeye (12:13b), lakini hata hivyo, ilimbidi Daudi kuketi katika karamu ya matokeo ya dhambi zake.

Matokeo

Nathani alilipitisha lile neno lake Bwana kwake Daudi: *'basi sasa upanga hautaondoka nyumbani mwako…nitakuondokeshea uovu katika nyumba yako*:(10a, 11a). Kwa sababu Daudi alitenda dhambi katika uhusiano wa kijamii, Mungu alimhukumu papo hapo. Kuanzia sura hii hadi nyingine, katika Samweli wa pili; tunaona unabii wake nathani ukitimika.

Kwanza kabisa, nabii alimwambia kwamba yule mtoto ambaye yeye na Bath-sheba watamzaa lazima atafariki. Na kwa siku sita usiku na mchana, Daudi akafunga kula na kunywa, akilala mbele zake Mungu. Lakini yule mtoto alizidi tu kuwa mgonjwa. Na katika siku ya saba, yule mtoto akafa. Daudi alifahamu jambo hili, aliinuka, akaoga, akajipaka mafuta akabadili mavazi yake, akaingia nyumbani mwa Bwana, akasali; kisha akaenda nyumbani kwake, na alipotaka wakamwandalia chakula, naye akala. Tabia yake iliwashangaza sana watumishi wake, lakini Daudi akaeleza kwamba, mwanawe akiwa bado yupo hai, kulikuwepo na taswishi kwamba Mungu angemrehemu na kumponya. Lakini kwa kuwa alifariki, Daudi alisema kwamba hakuna jambo ambalo angelitenda ili kumrudisha huku akiongeza kwamba*, 'Mimi nitakwenda kwake lakini yeye hatanirudia mimi.'* (12:23).

Iaonekana kwamba Mungu anapomchukua mtoto mchanga, hakuna shaka ye yote kwamba umilele wake upo wapi. Daudi aliyaeleza matumaini hayo alipokuwa akisema, 'Mimi nitakwenda kwake.' Hebu linganisha tabia hii ya Daudi pamoja na huzuni yake iliyokuwa nyingi wakati alipolipokea neno kuhusu kifo cha mwanawe, Absalomu hapo baadaye katika hadithi kuhusu kuadhibiwa kwake Daudi.

Tunaposoma sura ya 13 na sura zinazofuatia baadaye, tunavumbua kwamba matokeo ya dhambi yake Daudi yaliendelea. Mwanawe Daudi aitwaye AmnonI alimnajisi dada yake wa kambo jina lake Tamari. Baada ya tukio hilo, Absalomu mwanawe Daudi, ambaye alikuwa nduguye Tamari kwa mama mmoja na mboni ya macho yake Daudi, alimuua Amnoni na kukimbia kuishi kama mkimbizi. Na kwa maombezi na utetezi wake Yoabu, Absalomu aliruhusiwa kurudi na kuishi huko Yerusalemu. Lakini ingawaje Daudi alimruhusu Absalomu kurudi, yeye alikataa kukutana au kumwona yeye.

Daudi alitamani kushirikiana na mwanawe Absalomu, lakini alishindwa kabisa kumsamehe na kurudisha ushirika wao pamoja (14:24). Huku akiwa ametengwa mbali na mwenye uchungu, Absalomu aliandaa mapinduzi kinyume cha babake huku baadaye akimfukuza kutoka Yerusalemu. Pamoja na usaliti wake huyu Absalomu, alipewa usaidizi kutoka kwake mshauri mkuu aliyeaminika Ahithofeli. Yeye alimshauri Absalomu kumchokoza babake Daudi kwa kuwachukua masuria wake kumi na kulala nao juu ya paa machoni pa Israeli wote. Na kwa kusikitisha mno, Absalomu akalitenda jambo hilo lenye uovu mwingi kutokana na ushauri wake Ahithofeli.

Daudi alipoipata habari kuhusu tukio hilo- kwamba mtu ambaye alikuwa rafiki yake, na ambaye alikuwa kama baba kwake yeye, alikuwa amemshauri mwanawe kuwavamia wale wanawake wasio na kinga ye yote–akaiandika Zaburi 55. Soma Zaburi 55 na utaona kwamba moyo wake Daudi ulijawa na hofu kuu. Unaweza pia kusoma kuhusu janga hili lote katika maisha yake Daudi katika 2 Samweli 11-12.

Pamoja na yale yote huyu Absalomu aliyotenda, wakati vita vilipokuwa karibu kipiganwa kati ya mashujaa wake Daudi na jeshi la Israeli chini ya uongozi wake Absalomu, Daudi alilionya jeshi lake lisije likamjeruhi mwanawe Absalomu. Pigo kuu ambalo Mungu alimpiga Daudi ni wakati alipoupokea ujumbe kwamba Absalomu ameuawa. Hebu kwa mara nyingine tazama tofauti ambayo ipo kuhusu jinsi alivyo kumbana na kifo chake yule mtoto mchanga na kifo chake Absalomu. Absalomu alipouawa, huzuni yake Daudi ilikuwa nyingi mno. Alisema kwa kurudia tena na tena, '*Mwanangu Absalomu! Mwanangu Absalomu! Ee mwanangu! Ee mwanangu Absalomu! Laiti ningalikufa badala yako, Absalomu, mwanangu, mwanangu.1'*(18:33).

Absalomu alikuwa ameanza mapinduzi kinyume cha babake, lakini ni kwa sababu gani Daudi alikumbana na janga hili kwa njia hiyo? Tofauti na kifo chake mwanawe mdogo, Daudi, asingelisema kwake Absalomu kwamba, *'Mimi nitakwenda kwake*.' Yamkini labda hii ndiyo sababu ilimfanya huyu Daudi kuwa na huzuni kuu kwa ajili yake Absalomu. Na inawezekana kwamba, pia Daudi aliamini kuwa kifo chake Absalomu kilitokana na dhambi zake mwenyewe (yaani Daudi) kwa hivyo, alitumaini mambo yangelikuwa hivyo vingine.

Unaposoma hadithi kuhusu dhambi yake Daudi, na hasa matokeo ya dhambi yake, utatambua kwamba hakuna ye yote miongoni anayeweza kunusurika kuanguka (1 Wakorintho 10:12,13). Kumbuka kwamba Daudi alituonyesha sote jinsi ya kukumbana, kuanguka na kurekebisha

tabia zetu. Hivyo basi kutilia maanani maneno yake Bwana wetu Yesu Kristo aliposema kwamba, *'Enenda zako; wala usitende dhambi tena.'* (Yohana 8:11).

SURA YA KUMI NA MOJA.

Baraka Zilizo Katika Msamaha

Lengo kuu katika uchuguzi wetu wa Biblia kwa neno moja ni 'Kuambatishana.' Ningependa kukuonyesha jinsi vitabu vya Biblia vinavyohusiana kimoja kwa kingine, au umoja uliopo katika Biblia. Kwa mfano, baada ya kukagua vitabu vya kihistoria, unapofikilia vile vya manabii, utatambua kwamba tayari una msingi wa kihistoria jinsi ambavyo hawa manabii wakuu walivyoishi, kuhubiri, na kuteseka na hata kufa. Maandiko ya kihistoria yanakutayarisha wewe kukielewa kitabu kikuu katika Biblia, Zaburi na hasa Zaburi zake Daudi.

Moyo wake Daudi Katika Zaburi

Zaburi zake Daudi na 2 Samweli 11-18 zinaambatana pamoja kkwa halia ya kuvutia mno. Katika zaburi ambazo ziliandikwa nyakati za maisha yake, tunafikia kufahamu ukuu wake Daudi ingawaje katika maisha yake; huu ndio wakati ambao yeye alipata kushindwa kitabia na kiroho.

Zaburi Tatu

Daudi alipotoroka na kwenda nyikani ili kumkwepa Absalomu, mtu aitwaye Shimei alimlaani (2 Samweli 16:5-8). Jenerali wake Daudi alisema*, 'Mbona mbwa mfu huyu amlaani Mfalme bwana wangu? Na nivuke, nakusihi, nikaondoe kichwa chake.'* (9) Lakini Daudi akamjibu, *'Mwacheni alaani, kwa sababu Bwana ndiye aliyemwagiza.'* (11b).

Huku Daudi akitoroka kutoka Yerusalemu, aliandika Zaburi 3, ambayo inaanza hivi: *'Bwana watesi wangu wamezidi kuwa wengi, ni wengi wanaonishambulia, Ni wengi wanaoiambia nafsi yangu, Hana wokovu huyu kwa Mungu.' (1-2).* Hivi ndivyo Shimei alivyosema wakati alipomlaani Daudi na kumrushia mawe. Lakini Daudi alizidi kuandika (Na hapa ndipo alipodhihirisha jinsi alivyokuwa mtu mwenye kumcha Mungu), *'Na wewe, Bwana, U ngao yangu pande zote, Utukufu wangu na mwinua kichwa changu. Kwa sauti yangu namwita Bwana naye aniitikia toka mlima wake mtakatifu.'* (3-4).

Huku akiyatazama maisha yake ya hapo awali, Daudi angeliweza kuona ncha za miujiza – majibu kwa maombi –yakimjia katika njia yake. Na hii ilimpa yeye ujasiri nayo imani ya kumtumainia Mungu kwa wakati ule na wakati ujao.

Zaburi Nne

Zaburi hii ya nne inalingana na kipindi cha maisha yake Daudi. Yeye anatueleza kuwa hisia zetu zimo kwenye hatari na mbano wa kimaisha kiasi kwamba tunakosa, inawezekana kwamba sisi tuna jukumu kubwa itakikanayo kufanywa ambayo inahusika na kutenda jambo jema. Usiku wa manane wakati usingizi ulipomtoroka, yeye alifanya nadhiri ndani ya moyo wake *'kuzitoa dhabihu na kumtumainia Bwana' (5).* Motisha yake kwa kutenda yaliyo mema ilitokana na watu waliomzingira: *Ni nani awezaye kutuonyesha yaliyo mema?*' (6) Sote tumezingiriwa na watu ambao wanamtafuta mtu ambaye atalitenda lililo njema. Wao kilio chao ni pamoja na gharama ambayo tunailipa katika kulitenda jambo lililo njema, hubarikiwa sana na kumgeukia Mungu kwa yale wanayoyaona.

Zaburi Ishirini na Tatu

Katika Zaburi 23:3, Daudi asema hivi, *'Hunihuisha nafsi yangu.*' Wakati Bwana ametufanya kulala chini na kutambua kweli kwamba sisi tu kondoo naye ndiye mchungaji wetu, sisi huinuka tena. Lakini wakati sisi tunapoichukua nafasi yake na kujifanya kuwa tu wachungaji, yale majani mabichi hukauka na kuwa rangi ya hudhurungi, ilhali yale maji matulivu hufanyika kuwa na tufani kuu, huku kikombe chenye kufurika kikifanyika kuwa kavu. Tunaposahau ni nani aliye mchungaji au ni nani aliye kondoo, huwa tunahitaji kuhuishwa.

Je, Mungu hutuhuisha vipi? Yeye ni mwenye matendo. Daudi alilielezea hivi, *'Yeye huniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.'* (3b). Ufufuo ni zaidi ya kuenda mbele Kanisani wakati wa maombi. Ni zaidi ya ujuzi wa maombi kwenye madhabahu au kwenye mimbara. Mungu husema, *'Sikiza, hivi ndivyo mimi nataka kukuhuisha wewe. Njoo utembee katika njia za haki kwa kipindi cha miaka kadha. Na huku unapotembea katika njia za haki, hizo njia zitakuhuisha nafsi yako.'*

Hili ndilo jambo ambalo tunaliona likitokea katika maisha ya Daudi katika 2 Samweli 11-18. Daudi alijitolea kwake Mungu na kusema*, 'Mimi nitakuja na kutembea katika njia za haki kwa ajili ya*

jina lako.' Wakati Daudi alipokumbana na adhabu ya Mungu, na matokeo ya dhambi yake kwa kutembea katika njia za haki, Mungu aliihuisha nafsi yake.

Daudi alikuwa mfalme kwa muda wa miaka arobaini–kwa miaka kumi na sita kabla ya kutenda dhambi, na miaka ishirini na nne baada ya Mungu kumrudishia ufalme wake na kuihuisha nafsi yake. Lakini kuhuishwa huko kulikuja tu wakati alipotembea kwenye njia za haki kwa kuziungama, kutubu dhambi pamoja na kujitoa mwenyewe ili kuifuata njia yake Bwana.

Je, wewe unahitaji kufanya toba ya kweli, na maungamo kuaminika? Au kwa maneno mengine, je, unafahamu jinsi ya kutokufaulu kwenye fanisi? Katika upendo wote na kweli ninaweza kukushauri kwamba hautaweza kufahamu baraka iliyo katika msamaha hadi wakati utakapofuata mfano wake Daudi na kuziungama dhambi zako kwake Mungu. Kumbuka, toba inamaanisha kukubali yale ambayo Mungu mwenyewe ananena kuhusu dhambi zako. Nakupa changa mto upate kusoma Zaburi 32, 51, 55, 23 na kuyafanya maneno yake Daudi kukuongoza katika toba. Halafu kama yeye, ushuhuda wa baraka yake Mungu ya rehema ya msamaha wake.

Kuimba Nyimbo za Msamaha

Je, umewahi kujiuliza hivi, 'Nawezaji kufahamu kwamba dhambi zangu zimesamehewa?' Wengine husema kuwa unawaweza kufahamu kwa kuwa Biblia inasema hivyo : *'Biblia inasema, nami naamini, na hivyo basi yatosha.'* Lakini ipo njia nyingine ambayo wewe unaweza kufahamu kwamba dhambi yako imesamehawa: Wakati Mungu anapoitoa hatia ndani yako.

Siku ya leo washauri wengi wa kiakili na hisia (*Therapists)* hukumbana na shida hii ya hatia kwa njia nyingine. Wao husema, *'hakuwezekani kuwa na kitu kama hatia kwa kuwa hakuna kitu kilicho kizuri au kibaya. Hakuna jambo ambalo wewe haustahili kulitenda. Na hakuna ambalo unahitajika kulitenda. Hakuna tabia yenye kukubalika kabisa kote kule. Hatia ni ya watoto wadogo, kwa sababu ni watoto ambao hukubali kuambiwa yale yanayokubalika na yale yasiyokubalika. Usimruhusu mtu ye yote kukueleza kwamba yale unayoyatenda ni maovu.'* Ni jambo la kushangaza kuona kwamba kuna watu wengi sana hujaribu kuitatua shida yao ya kujihisi kuwa na hatia kwa njia hiyo.

Na kinyume na hayo, Daudi kwa dhati asema hivi, *'mimi nina shida ya hatia kwa kuwa mimi ni mwenye hatia. Mimi nina shida ya hatia kwa kuwa mimi nimetenda dhambi.'* Suluhisho lake Mungu

kwa shida yetu ya hatia ni kwa kuungama kwamba sisi tu wenye hatia, na kwamba tumeitenda dhambi. Tunaonyesha kwamba tunafahamu na kuamini suluhisho lake Mungu kwa shida ya hatia yetu wakati tunapozitoa dhabihu za haki zenye kudhihirisha maungamo na toba yetu, pamoja na kuiweka tumaini yetu kwake Bwana. Ndipo papo, tunaweza kuwa na ushuhuda wa baraka ya msamaha, kwa kuwa hatia yetu itakuwa imeondolewa.

Zaburi 51-siyo tu maungamo yake Daudi kuhusu dhambi yake, bali kwamba ni dirisha ambalo tunaweza kuuona ukuu wa huyu mtu. Katika Zaburi 51, hebu yatazame mambo kadha: *'Tazama, wapendezwa na kweli iliyo moyoni; nawe utanijulisha hekima kwa siri.'*(6), na jibu kwa ombi hilo, Mungu alimpa Daudi ufunuo, naye akaandika*: 'Na dhambi yangu I mbele yangu daima……tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu; mama yangu alinichukua mimba hatiani.'* (3b, 5).

Linalofuatia, hebu tazama ombi kuu lake Daudi: *'Ee Mungu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu.'* Neno hili 'kuumba' katika msitari huu ni 'bara', katika lugha ya Kiebrania, ambalo humaanisha, 'Kuunda kutoka kwa utupu.' Neno hili latumika mara tatu peke yake katika kitabu cha Mwanzo sura ya kwanza, na linatumika kwa mara nyingine hapa katika Zaburi 51:10, ambapo linamaanisha kwamba Daudi alikuwa akiuliza kwa hakika kwamba*, 'Hauna lo lote lile lakutenda kazi nalo. Nakuomba ukiumbe kitu kutoka kwa utupu. Weka kitu ndani mwangu katika kina cha utu wangu ambacho hakikuwepo hapo mwanzoni nilipozaliwa. Ni lazima ulitende tendo la miujiza katika utu wangu wa ndani. Hili tu ndilo tumaini ambalo ninalo katika kuishi maisha yenye kukutukuza wewe.'*

Jibu kwa ombi hilo ni lile ambalo Agano Jipya linalitaja kama 'uzao upya.' Yesu asema, 'Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, hamna budi kuzaliwa mara ya pili,'- au, kwa maneno mengine, Wewe wahitaji tendo lingine la uumbaji katika moyo wako (Yohana 3:6-7).

Mitume wanataja uzao huu mpya 'Kuumba'*: Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa <u>kiumbe</u> kipya; ya kale yamepita tazama!'* (2 Wakorinho 5:17). Mungu ameumba kitu katika kina chake mwanamume au mwanamke ambaye amezaliwa kwa mara ya pili. Daudi alikuwa na mwangaza wa unabii wakati alipokuwa akiomba ombi hili yapata miaka elfu moja kabla ya Yesu kusema, *'Ni lazima uzaliwe mara ya pili.'*

Pia unaweza kuona shauku hii yake Daudi kutaka kuhuishwa: *'Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya wepesi. Nitawafundisha wakosaji njia zako, na wenye dhambi watarejea kwako.'*(Zaburi 51:12-13). Daudi alilipenda neno lake Mungu – alipenda kulihubiri, na hata kuliimba. Yeye alitaka kuwaongoza wenye dhambi wengine kumrudia yeye aliye mwanzilishi wa Neno hilo jinsi ambavyo alikuwa ametenda nyakati za hapo mbeleni.

Na mwishowe, tunaona mwangaza usio wa kawaida ambao Daudi anaudhihirisha hapo mwisho wa Zaburi hii: '*Maana hupendezwi na dhabihu, au ningeitoa, Wewe huridhii sadaka ya kuteketezwa.*'(16). Kumbuka tulipokuwa tukijifunza kuhusu Hema la kukutania huko nyikani? Watu wangewapeleka wanyama hadi kwenye Hema la Ibada na kuwateketeza kama dhabihu kwa ajili ya dhambi zao. Namna ya mnyama au hesabu yake ilitegemea dhambi yake mtu pamoja na uwezo wake kiuchumi.

Daudi alifahamu kwamba yeye angaliweza kulipeleka kundi nzima la wanyama katika Hema la Ibada, lakini pia alifahamu kwamba Mungu hakutaka jambo hilo. Na kwa maneno mengine Daudi alisema, *'Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau.'* Neno hili 'kuvunjika' linamaanisha, 'Sikitiko kuu kwa dhambi.' Daudi alisema, 'Hilo ndilo ambalo wewe walitaka, Mungu.' Hivyo basi akaomba, *'Nivunje mimi katika kina cha utu wangu. Niponye mimi katika utu wangu. Uniumbie mimi kitu katika kina cha utu wangu, ambacho hakikuwepo nami wakati nilipozaliwa kimwili, na hivyo basi, mimi nitaishi maisha ambayo yatakutukuza wewe.'*

Hebu rudia tena pamoja nami kwa kusema, ikiwa wewe umetenda dhambi na haufahamu jinsi ya kuungama dhambi yako, na unahitaji kufanywa upya katika moyo wako, njoo katika Zaburi 51. Iruhusu hii Zaburi iwe ombi lako la maungamo na toba. Utalifanya jambo la kuvutia la toba na maungamo ya dhambi yako ikiwa utatenda hivyo.

SURA YA KUMI NA MBILI.

Kweli Tatu za Dhambi na Kweli Tatu za Wokovu

Ningependa kama ungalikuwa na sura moja ya somo lake kuhusu dhambi yake Daudi. Labda unadhani kwamba tunatilia jambo hili mkazo zaidi, lakini ni kwa kuwa maandiko yenyewe yanatilia mkazo dhambi yake Daudi. Tunahitajika kujaribu kuvumbua sababu gani Mungu alilipatia nafasi kubwa katika Samweli wa

pili dhambi yake Daudi. Hii ni kwa sababu tupate kujifunza masomo ya kiroho ambayo Mungu anataka sisi kujifunza kuhusu dhambi na kuyatenda tunayojifunza wakati tunapoitenda dhambi.

Somo la Ziada Kuhusu Dhambi

Somo lenye umuhimu mno ambalo tunaweza kulipata katika hadithi kuhusu dhambi yake Daudi ni jinsi yeye alivyokumbana na shida ya kuwa na hatia ndani yake. Hebu tazama mfano huu.

Akili yake mwanadamu ina sehemu mbili: Moja inajulikana kama (*Conscious)* kwa ufasaha na ile nyingine *(Subconcious)*. Sisi huwa tunazozana na mawazo yetu yasiyoambatana vema. Katika akili zetu zenye kutambulikana, yaani *conscious*, sisi huwa na wazo kama, '*Bwana ndiye mchungaji wangu.*' Lakini kwa wakati mwingine, katika sekunde thelathini zijazo, huwa tunaingiwa na hofu. Nayo matokeo yake huwa vidonda vya tumbo yaani *(Ulcers*) au Msokoto ya tumbo *(Colitis*). Hatuhitajiki kuwa na hofu kwa kuwa Mungu ndiye mchungaji wetu. Hata hivyo, sisi hufanya hivyo. Je tunawezaji kukumbana na mawazo haya yenye kipingana?

Sisi hujenga ukuta katika akili zetu na kuyagawanya hayo mawazo yenye mzonzo yasiyoambatana pamoja katika vifungu viwili. Katika kifungu kimoja, tuna imani nasi husema, '*Bwana ni mchungaji wangu.'* Tunaposema hivyo, hatujiruhusu kukumbuka kwamba tuna vidonda vya tumbo kwa sababu ya hofu yetu. Na katika kifurushi kile kingine kilichoko katika akili zetu, sisi hujawa na hofu hata hatujikumbushi kana kwamba tunayo imani! Jambo hili hutufanya kuwa na dhana isiyo badilika ya vifurushi viwili katika 'mzonzo ulio ndani ya roho zetu' yaani *('Spiritual Schizopheria').*

Pingamizi au mzonzo huu wa kiroho siyo jambo kuu katika sehemu ya akili ambayo inatambulikana kwa ufasaha. Lakini katika nia yetu ya ndani isiyotambulikana, ni yenye umuhimu mno. Hii ni kwa kuwa kila wazo ambalo lipo katika sehemu ya akili inayotambulikana hukaa katika ile isiyotambulikana kwa milele. Hivyo basi mzonzo wetu huingia katika nia au akili yetu ya ndani isiyotambulikana kwa urahisi na kujenga boma ambalo halionekani lenye kuwa na mzonzo. Hii inaweza kuwa shida kuu kwa kuwa nia isiyotambulikana kwa ufasaha ni kama kikombe. Kinapojazwa na mzonzo huo, huwa kinatuma ishara katika miili yetu, nasi huanza kuadhirika kiafya na ishara hizo zinazoonekana.

Maandiko hutueleza sisi kwamba tusiubane mzonzo bali tuusuluhishe. Madaktari wa akili na hisia wakubaliana, lakini wakati mwingi wao huzitumia njia tofauti katika kusuluhisha mzonzo.

Suluhisho zao za kilimwengu huwa ni kuwapeleka watu mbali na dhamana kuu katika maisha yao hasa zile za kitabia ambazo hupingana na tabia zao. Lakini maandiko hutufundisha kwamba kuna kitu kama wema na ubaya. Nasi ikiwa tuna kanuni dhabiti kuhusu stahi na wema kwa sababu sisi tunaamini kanuni dhabiti kuhusu stahi na tabia yakubalikana. Na ikiwa maisha yetu hayaambatani na kanuni ile dhabiti kuhusu stahi au tabia bora, sisi hujifanya kuugua.

Maandiko hutushauri kusuluhisha mzonzo wetu kwa njia hii: Kwa kuwa taa ya mwili ni macho, ikiwa mtazamo, au mwelekeo wa kiakili ni ule ambao Mungu anataka uwe, sisi huishi kwa jinsi ambavyo tunavitizama vitu, nayo miili yetu hujawa na nuru sehemu zote. (Tazama Mathayo 6:22). Na kwa maneno mengine, sisi husuluhisha mzonzo kulingana na vile tunavyoamini.

Daudi anatushauri kusuluhisha shida ya hatia yetu wakati tunapotambua kanuni yake Mungu kuhusu yale yaliyo mema na yale yasiyo mema, hata kama kanuni hiyo inatushawishi kuwa wenye dhambi na kutuhukumu dhambi yetu. Tunapoungama dhambi yetu, Mungu atatufanya upya katika nafsi zetu. Hili ndilo jambo kuu linaloweza kutendeka kwetu ambalo tunalipata katika hadithi hii kuhusu dhambi yake Daudi.

Kweli Tatu Kuhusu Dhambi

Jambo lingine ambalo tunalipata na kujifunza katika sura hii kuhusu hadithi mbaya yake Daudi kuhusu maisha yake ni kwamba dhambi ina matokeo mabaya. Katika 2 Samweli 11-18, Daudi alibiidika kula karamu ya matokeo machungu. Hadithi yake kwa hakika inatuonyesha kweli tatu kuhusu dhambi na kweli tatu kuhusu wokovu. Hebu tutazame upande wa dhambi kwanza.

Adhabu ya Dhambi

Jambo la kwanza, ni kwamba dhambi ina adhabu yake. Dhambi kwa wakati wote huongoza katika adhabu ya baadaye na wakati uliopo sasa. Na hii ndiyo sababu ilimbidi Mungu kuharisha mbinguni na kumtuma Yesu Kristo ulimwenguni huu. Njia ya kipekee tunayoweza kuondoa adhabu ya dhambi (Jehanum) katika maisha yetu ni kuamini kifo chake Yesu Kristo juu ya msalaba. (Tazama Yohana 3:16).

Hata hivyo, mara nne kwa tano 4/5 ya wakati maandiko yanapotumia neno wokovu, halitumii kwa wakati ujao kuhusu adhabu ya dhambi bali kwa kuondolewa kwa adhabu iliyopo wakati huu ya dhambi. Kwa mfano, sisi huokolewa kutokana na adhabu ya maisha yenye uharibifu. Wakati Yesu

alipozungumza kuhusu jehanum, alitumia neno la Kiyunani au Kigiriki 'Gehenna.' Gehenna palikuwa ni mahali pakubwa ambapo takataka kutoka mji wa Yerusalemu ilikuwa ikitupwa'. . . *'Na ambapo funza wao hafi, na moto wake hauzimiki.'* (Marko 9:44). Watu walipofikiria kuhusu Gehenna, wao walikuwa wakiwaza juu ya taka. Yesu alifundisha kwamba taka lilikuwa ni uhakika muovu na mkuu uliopo Jehanum.

Adhabu nyingine ya dhambi ni kuhusu kufungwa. Watu hawatendi kama wapendavyo kutenda; ila wao hutenda yale ambayo ni lazima watende, na yale walazimishwayo kutenda. Watu wanatawaliwa na kuhangaishwa na tabia ambazo Biblia inazitaja kama dhambi. Wokovu huwaweka watu huru kutokana na utumwa wa dhambi. (Tazama Yohana 8:30-35; Mathayo 1:21).

Mshahara wa dhambi

Jambo la tatu, ni kwamba dhambi ina mshahara mkuu. Paulo anatuambia, *'Mshahara wa dhambi ni mauti.'* (Warumi 6:23). Paulo alimaanisha sio tu kwamba ni mauti ya kimwili bali pia karamu ya matokeo – ile chungu ambayo mwenye dhambi hula mwishowe. Dhambi ina makofu na mawaa yake, na baadhi ya mawaa mengine na makofu yake huwa hayawezi kubadilishwa au kupinduliwa.

Kweli Tatu Kuhusu Wokovu

Jinsi ilivyo kitambaa cheusi cha mhuzi wa almasi na dhahabu kinavyoifanya almasi na lulu kumetameta, giza kuu ya mshahara wa dhambi na uwezo wake huzifanya kweli tatu kuhusu wokovu kung'ara zaidi.

Yesu Ameondoa Adhabu ya Dhambi

Kwanza, Yesu Kristo ameiondoa adhabu ya dhambi. Maandiko yanataja hii kuwa 'Injili' au 'Habari Njema.' Kama vile Yesu alivyomwambia Nikodemu, 'Mimi ndimi Mwana wa pekee wake Mungu, Mimi ndimi suluhisho la pekee, nami ndimi mwokozi wa pekee wake Mungu.' (Tazama Yohana 3:14-18). Unaposikia kwa uhakika yale ambayo Yesu aliyanena, utatambua kwamba alifungua njia ambayo ilikuwa imefungwa katika dini zingine zote. Aidha, wewe umwamini Yesu au usimwamini. Hili ni tamko kuu na lenye kanuni ya imani ambalo Yesu aliwahi kulitamka mwenyewe.

Roho Mtakatifu Aweza Kushinda Uwezo wa Dhambi

Pili, ni kwamba, Roho Mtakatifu anaweza kutawala uwezo wa dhambi ndani ya maisha yako na yangu. Mtume Yohana anatuambia katika 1 Yohana 4:4, *'… Yeye aliye ndani ya yenu ni mkuu kuliko yeye katika dunia.'* Kando ya nguvu zake Mungu, hamna nguvu zingine ulimwenguni kote kuliko nguvu za dhambi, za uovu na zake Shetani. Lakini habari njema ni kwamba uwezo wake Mungu ni mkuu kuliko ule wake Shetani, uovu na dhambi! Mtume Paulo asema wakati sisi tunapoipokea neema yake Mungu, hufanyika kuwa zaidi ya washindi juu ya uwezo wa dhambi katika maisha yetu. (Linganisha Warumi 8:37-39).

Haki yake Yesu Huondoa Dhambi yetu Mbele yake

La tatu kuhusu kweli ya wokovu ni lenye kutatanisha zaidi, kwa kuwa huhusika na mawaa ya dhambi na makofu yake pamoja na adhabu yake. Machoni pake Mungu, hata mawaa ya dhambi huondolewa na kuoshwa wakati wa msamaha. Na kama vile Daudi alivyoandika katika mojawapo ya Zaburi yake: *'Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.'* (Zaburi 103:12; Mika 8;19). Neno 'kufanywa haki' ni neno lenye kuvutia sana katika Biblia. Linamaanisha kutubu na kuungama dhambi yetu. Kulingana na vile Mungu anavyohusika, dhambi yetu haipo kabisa na wala haikutendeka! Dhambi yetu inasamehewa na kuondolewa kabisa. Ni kana kwamba haikutendeka hata kidogo.

Lakini hata hivyo, kufanywa haki huja kwa njia mbili. Wakati mwingine mawaa au makofu ya dhambi hayawezi kubadilishwa katika hali ya kibinadamu. Kama mtu akimuua mwenzake na baadaye kumwamini Yesu Kristo, machoni pake Mungu, ni kana kwamba yeye hakuwahi kuitenda dhambi wala kutenda kitendo cha mauaji. Lakini je, imani yao katika Yesu yaweza kumaanisha kwamba wao waweza kuachiliwa huru? La Hasha. Yangalipo matokeo ya adhabu ile.

Mchungaji mmoja alimtembelea mzee moja mwenye umri wa miaka themanini na tatu. Yeye alikuwa ameokoka akiwa na umri wa miaka themanini na miwili, jambo ambalo siyo ya kawaida. Baada ya kuokoka kwake, ambako kulikuwa kwa kweli, mke wake alimwita yule mchungaji na kusema, *'Ni lazima uje na kuzungumza na mume wangu. Kile anachofanya ni kuketi akilia machozi tu, naye hataki kuzungumza kuhusu hilo jambo.'* Na hivyo huyo mchungaji akaandamana na yule mke wa mzee. Huyu mzee alipokuwa amejituliza, alisema, *'Wanangu! Wanangu! Wanangu!'* Yule mchungaji akauliza, *'Mbona unawataja watoto wako?'* Yule mzee akaanza kumweleza huyu mchungaji jinsi alivyowatendea mabaya hawa wanawe. Wawili kati yao walikuwa katika hospitali

wakiwa wagonjwa wa akili, na kulingana na maoni yake, yeye ndiye aliyehusika katika hali hiyo. Huyu mzee kwa hakika alikuwa tayari ameokoka na mbele ya macho yake Mungu yeye hakuwa na mawaa au makofu, wala adhabu. Lakini hata hivyo, magofu ya watoto wake yalikuwa ya hakika hata wakati ule.

Yapo mambo ambayo sisi hatuwezi kuyabadilisha. Ni kama mayai yaliyo korogwa au kupigwa. Thamani ya dhambi ni kubwa mno, na magofu yake hayazoleki. Na hii ndiyo sababu mtume Yohana anaandika katika waraka wake wa kwanza: *"Ninawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi.'* (1 Yohana 2:1).

Ni mzaha mkuu wa kidini kuwapa vijana wachanga fikira kwamba kipo kitu cha kufurahisha au cha kupendeza kuhusu dhambi. Hamna cho chote chema kuhusu dhambi au matokeo yake. Mungu huidhihirisha neema yake na rehema zake kama tukikumbana na matokeo ya dhambi jinsi Daudi alivyofanya. Mungu aweza kuponya magofu, lakini mawaa na magofu hayawezi kubadilika. Na hii ndiyo sababu maandiko husema kwamba ni vyema kama mtu asipoitenda dhambi. 'Sikuhukumu wewe,' Yesu akamwambia mwanamke ambaye alifumaniwa katika usherati; lakini akazidi kusema, kwa kuwa alimpenda yule mwanamke, 'Usitende dhambi tena.' Yohana 8:11). Usimruhusu mtu ye yote kuwashawishi watoto wako kwamba kipo kitu chema na chakupendeza katika kuishi dhambini na kuokolewa kutoka maisha ya dhambi. Ni bora zaidi kutokuitenda dhambi.

Ipo dhambi miongoni mwa watu ambao wanasema kwamba wao ni wanafunzi wake Yesu Kristo siku ya leo. Mungu anataka sisi wote, kuiptia hadithi ya dhambi yake Daudi, kuyasikiza maneno yake Yesu siku ya leo*: 'Nenda na usifanye dhambi tena.*'